**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA (PPRA)**

# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA UPENDELEO KATIKA UNUNUZI WA UMMA, 2025

**JANUARI 2025**

***Tarehe ya Kuanza Kutumika: 23 Januari, 2025***

**MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA UPENDELEO KATIKA UNUNUZI WA UMMA, 2025**

| Imeidhinishwa na | Cheo | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Bodi ya Wakurugenzi | Mkurugenzi Mkuu | | 22 Januari 2025 |


**Umetolewa na:**
*Mkurugenzi Mkuu,*
*Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma,*
*Tambukareli Dodoma,*
*3 Mtaa wa Ununuzi,*
*S.L. P 2865,*
*41104 Dodoma, TANZANIA*
*Barua pepe: dg@ppra.go.tz*
*Simu: +255 (0) 26 296 3854*
*Tovuti: https://www.ppra.go.tz*

## YALIYOMO


**ORODHA YA VIAMBATANISHO ........ vii**

**VIFUPISHO ........ viii**

**TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA ........ ix**

**UTANGULIZI ........ 1**

*Chimbuko ........ 1*

*Jina la Mwongozo ........ 2*

*Dhumuni ........ 2*

*Matumizi ya Mwongozo ........ 2*

*Tafsiri ya Maneno ........ 3*

**SIFA ZA UPENDELEO ........ 6**

*Sifa za Upendeleo ........ 6*

**MPANGO WA UPENDELEO NA UKOMO ........ 9**

*Upendeleo wa kitaifa ........ 9*

*Upendeleo wa Kipekee kwa watu na kampuni za ndani ........ 12*

*Upendeleo wa Bidhaa za Ndani ........ 13*

*Upendeleo wa Kimkoa ........ 15*

**USHIRIKA, MKATABA MDOGO NA UBIA ........ 16**

*Matumizi ya Ushirika ........ 16*

*Uundwaji wa Ushirika ........ 17*

*Mahitaji ya Ushirika ........ 18*

*Kuwasilisha zabuni kwa Ushirika ........ 19*

*Wajibu dhidi ya Ushirika* ........................................................................................ 20

**UINGIAJI MKATABA MDOGO** ........................................................................................ **20**

*Mahitaji ya Uingiaji Mkataba Mdogo* ........................................................................................ 20

*Utaratibu wa kuingia Mkataba mdogo ulioteuliwa* ........................................................................................ 22

*Utaratibu wa kuingia mkataba mdogo na mkandarasi wa Ndani* ........................................................................................ 23

*Makubaliano ya Mkataba mdogo* ........................................................................................ 25

*Usimamizi wa Mikataba Midogo* ........................................................................................ 25

*Uundaji wa Ushirika au mkataba mdogo na Kampuni za kigeni* ........................................................................................ 26

**C: UBIA** ........................................................................................ **27**

*Uundaji wa Ubia* ........................................................................................ 27

*Uthibitisho wa Umiliki wa Hisa* ........................................................................................ 27

*Mchango wa Rasilimali* ........................................................................................ 28

*Upendeleo kwa Wabia* ........................................................................................ 28

**USHIRIKI WA WAZABUNI WA KIGENI KATIKA HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI** ............... **28**

*Ujumuishaji wa wataalamu na kampuni za ndani katika huduma za ushauri elekezi* .................... 28

*Uundaji wa Ushirika au Muungano katika mikataba ya ushauri elekezi* ........................................ 31

**KUJENGA UWEZO KWA WATU AU KAMPUNI ZA NDANI** ........................................................................................ **32**

*Utengaji wa zabuni kwa ajili ya kujenga Uwezo* ........................................................................................ 32

*Mazingatio ya Wastani wa Mauzo kwa Mwaka* ........................................................................................ 33

*Uzoefu wa kuzingatiwa kwa Makampuni ya Ndani* ........................................................................................ 34

**MASHARTI YA JUMLA** ........................................................................................ **36**

*Ushiriki wa wazabuni wa kigeni katika zabuni awali zilizotengwa kwa ajili ya wazabuni wa ndani* 36

*Ajira kwa mfanyakazi msaidizi wa ndani* ........................................................................................ 36

*Upendeleo kwa kampuni za ndani zinazounda ushirika na Kampuni nyingine za Ndani* ............. *37*

*Upendeleo kwa makampuni ya ndani yanayoingia mkataba mdogo wa kazi za ujenzi na makampuni mengine ya ndani*............................................................................................................ *38*

*Ukomo wa Upendeleo kwa Wauuzaji wa bidhaa, Washauri elekezi na watoa huduma zisizo za ushauri elekezi wa ndani wanaoingia mkataba mdogo na Wauuzaji wa bidhaa, Washauri elekezi na watoa huduma zisizo za ushauri elekezi wa ndani* ...................................................... *40*

*Upendeleo kwa kampuni mama za ndani* ........................................................................... *42*

*Malipo kwa kampuni za ndani* ........................................................................................... *42*

*Tathmini ya zabuni chini ya mipango ya upendeleo* ......................................................... *42*

*Mafunzo kwa wahitimu wanaojifunza kwa Vitendo* ........................................................... *43*

*Utatuzi wa Migogoro* ......................................................................................................... *45*

*Ufuatiliaji wa Mwongozo huu* ........................................................................................... *45*

*Mapitio ya Mwongozo* ....................................................................................................... *45*

**VIAMBATISHO** ................................................................................................................ **46**

**MAKUBALIANO YA USHIRIKA** ........................................................................................ **52**

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


Kiambatisho 1: Fomu ya Taarifa za Wanachama wa Ushirika

Kiambatisho 2: Fomu ya Kubainishwa Wanafaika wa Umiliki.

Kiambatisho 3: Tamko la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamiiTamko la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamii

Kiambatisho 4: Fomu ya Mfano ya Makubaliano ya Ushirika – Kampuni na mtu wa ndani

Kiambatisho 5: Fomu ya Mfano ya Makubaliano ya Ushirika – Kampuni na mtu wa ndani na wakigeni

Kiambatisho 6: Taratibu Za Kukokotoa Viwango Vya Ufaulu Kwa Mshauri Elekezi

Kiambatisho 7: Wastani Wa Mapato Kwa Mwaka

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| PPRA | - | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma |
| NeST | - | Mfumo wa Kielectroniki wa Ununuzi wa Umma Tanzania |
| BRELA | - | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| WMM | - | Wastani wa Mauzo ya Mwaka |
| TAESA | - | Mamlaka ya Huduma za Ajira Tanzania |
| AQRB | - | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi |
| ERB | - | Bodi ya Usajili wa Wahandi |

## TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA

| | |
|---|---|
| **Jina la Nyaraka** | Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Upendeleo Katika Ununuzi wa Umma, 2025 |
| **Toleo** | Toleo la Kwanza, Januari 2025 |
| **Namba ya Nyaraka** | PPRA/PSCD/MPS/25/05 |
| **Jukumu** | Menejimenti ya PPRA, Taasisi Nunuzi, Wazabuni |
| **Imeandaliwa na** | Menejimenti ya PPRA |
| **Uidhinishaji wa Kwanza (Toleo la Kwanza)** | Bodi ya Wakurugenzi PPRA, Januari 2025 |
| **Utekelezaji** | Taasisi Nunuzi, Wazabuni |
| **Dhumuni** | Kutoa Mwongozo kwa Taasisi Nunuzi wa namna ya kutimiza masharti ya Ununuzi wa Umma Endelevu kupitia utekelezaji wa mpango wa upendeleo kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni zake. |
| **Ni sehemu ya** | Miongozo ya Ununuzi wa Umma |
| **Nyaraka Nyingine zinazohusishwa** | Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni za Ununuzi wa Umma Tangazo la Serikali Na: 518 la Mwaka 2024 |
| **Usambazaji** | Bodi ya Wakurugenzi ya PPRA, Menejimenti ya PPRA, Taasisi Nunuzi na Wazabuni |

*Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Upendeleo katika Ununuzi wa Umma, 2025.*

| UTANGULIZI | | |
|---|---|---|
| 1. | **Chimbuko** | 1.1. Kwa mujibu wa Kifungu cha 130 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imepewa mamlaka ya kutoa Miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo au majukumu chini ya Sheria.<br><br>1.2. Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(2) (b) cha Sheria, ununuzi, ugavi na uondoshaji mali za umma utafanyika kwa namna itakayoongeza uadilifu, ushindani, uwajibikaji, uendelevu, matumizi sahihi ya fedha, ufanisi na uwazi. Aidha, Kifungu cha 5(3) (c), taasisi nunuzi, katika kutekeleza wajibu wake zitafanya jitihada za kufikia viwango vya juu vya haki, kwa kuzingatia uendelezaji wa viwanda vya ndani, maendeleo endelevu na uhifadhi wa mazingira.<br><br>1.3. Ununuzi wa Umma Endelevu unajumuisha nguzo za kiuchumi, kijamii na kimazingira, ambapo uwezeshaji wa makampuni madogo madogo, madogo na/au ya kati upo chini ya nguzo ya kiuchumi.<br><br>1.4. Kwa mujibu wa Kanuni ya 38 (4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2024, PPRA inatakiwa kuandaa mwongozo wa namna ya kutekeleza masharti ya upendeleo kwa watu na kampuni za ndani. Vifungu 56,57, 58, 59, 60, 61, 62, na 63 vya Sheria Sura 410, Taasisi Nunuzi zinatakiwa kutoa upendeleo kwa watu, kampuni za ndani na bidhaa |

| | | |
|---|---|---|
| | | zinazotengenezwa, kuzalishwa au kuchimbwa ndani ya Tanzania.<br><br>1.5. Kufuatia takwa la kisheria la kuandaa miongozo lililotajwa hapo juu, PPRA inatoa mwongozo wa utekelezaji wa mpango wa upendeleo katika ununuzi wa umma kwa Taasisi Nunuzi. |
| 2. | **Jina la Mwongozo** | 2.1. Mwongozo huu utajulikana kama Mwongozo wa Utekelezaji wa Mpango wa Upendeleo katika Ununuzi wa Umma, 2025. |
| 3. | **Dhumuni** | 3.1. **Dhumuni Kuu**<br>Kutoa Mwongozo kwa Taasisi Nunuzi wa namna ya kutimiza masharti ya Ununuzi wa Umma Endelevu kupitia utekelezaji wa mpango wa upendeleo kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni zake.<br><br>3.2. **Dhumuni Mahsusi**<br>a) Kutoa mwongozo wa taratibu zinazopaswa kufuatwa na Taasisi Nunuzi wakati wa kutekeleza mpango wa upendeleo katika mchakato wa ununuzi; na<br><br>b) Kuhakikisha ulinganifu wa utekelezaji wa mpango wa upendeleo katika ununuzi wa umma. |
| 4. | **Matumizi ya Mwongozo** | 4.1. Mwongozo huu utatumika kuanzia tarehe ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 4.2. Mwongozo huu utatumika wakati wa kutekeleza mpango wa upendeleo katika ununuzi utakaofanyika chini ya:<br>a) njia za ushindani wa wazi za kitaifa na kimataifa;<br>b) Ununuzi wenye thamani hadi shilingi bilioni 50;<br>c) Ununuzi chini upendeleo wa kipekee wa kimkoa;<br>d) Utaratibu wa Ushirika, Ubia, na Mkataba mdogo;<br>e) Utoaji tuzo kwa kampuni za kigeni zinazotaka kuingia mkataba mdogo kabla ya kusaini mkataba;na<br>f) Upendeleo kwa bidhaa zinazotengenezwa, kuzalishwa au kuchimbwa ndani ya Tanzania.<br><br>4.3. Mwongozo huu hautatumika katika upendeleo wa kuhamasisha ushiriki wa makundi maalum katika ununuzi wa umma. Upendeleo kwa makundi maalum utazingatia Mwongozo wa Ushiriki wa Makundi Maalum katika Ununuzi wa Umma, 2025 uliotolewa na PPRA. |
| 5. | **Tafsiri ya Maneno** | 5.1. Katika Mwongozo huu, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo: -<br><br>**“Bodi”** maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 22 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410.<br><br>**“Mkataba”** maana yake ni makubaliano yaliyoingiwa baina ya taasisi ya umma na mzabuni yanayotokana na utaratibu wa ununuzi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | **"Kampuni ya kigeni"** maana yake ni kampuni ambayo asilimia kubwa ya mtaji wa hisa zake inamilikiwa na raia wa nchi ya kigeni.<br><br>**"Mzabuni wa kigeni"** maana yake ni kampuni ambayo asilimia kubwa ya mtaji wa hisa zake inamilikiwa na raia wa nchi ya kigeni.<br><br>**"Serikali"** maana yake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br><br>**"Bidhaa za Ndani"** maana yake bidhaa zinazotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano na huduma zinazohusiana.<br><br>**"Zabuni yenye Bei ya Chini Zaidi iliyofanyiwa Tathmini"** maana yake ni zabuni yenye bei ya chini zaidi baada ya kuzingatia vigezo vyote muhimu vya upimaji vilivyokokotolewa ili mradi vigezo hivyo vimeainishwa katika nyaraka za zabuni.<br><br>**"Kiwanda cha Ndani"** maana yake ni kiwanda chochote chenye leseni, kilichopo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br><br>**"Kampuni ya Ndani"** maana yake ni kampuni ambayo asilimia kubwa ya mtaji wa hisa zake inamilikiwa na raia wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. |

| | | |
|---|---|---|
| | | **"Ubia"** maana yake ni uhusiano uliopo kati ya watu wanaofanya biashara kwa pamoja kwa madhumuni ya kupata faida.<br><br>**"Hisa zilizolipiwa"** maana yake ni hisa ambazo mbia amelipa kikamilifu.<br><br>**"Makisio ya Gharama"** maana yake ni kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kazi au gharama ambazo haziwezi kutabirika, kufafanuliwa, au kuelezwa kwa ukamilifu wakati nyaraka za zabuni zinapotolewa.<br><br>**"Fedha za Umma"** maana yake ni rasilimali fedha zilizotengwa kupitia michakato ya kibajeti kwa taasisi nunuzi, ikijumuisha Mfuko Mkuu, misaada na mikopo iliyowekwa kwa ajili ya matumizi ya taasisi nunuzi na wafadhili wa ndani au wa nje na mapato yaliyozalishwa na taasisi nunuzi.<br><br>**"Msajili"** maana yake ni Msajili chini ya Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara, Sura ya 213 au Sheria ya Makampuni, Sura ya 212.<br><br>**"Kanuni"** maana yake ni Kanuni za Ununuzi wa Umma, (TS.Na. 518) la 2024.<br><br>**"Upendeleo wa Kimkoa"** unamaanisha upendeleo unaotolewa kwa wazabuni, wakandarasi na watoa huduma wanaoendesha shughuli zao za biashara ndani ya Mkoa husika Tanzania. |

| | | |
|---|---|---|
| | | **"Mkataba Mdogo"** maana yake ni makubaliano ya kisheria kati ya mkandarasi mkuu/mtoa huduma/mshauri elekezi na kampuni au mtu wa ndani kwa ajili ya kutekeleza sehemu ya majukumu ya mkataba wa mkandarasi mkuu/mtoa huduma/mshauri elekezi na Taasisi Nunuzi.<br><br>**"Mzabuni"** maana yake ni mtu yeyote, kampuni au kikundi cha watu ambao wanashiriki au wanakusudia kushiriki kwenye mchakato wa ununuzi kwa lengo la kuwasilisha zabuni kwa ajili ya kuingia mkataba na inajumuisha muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, mtoa huduma au mnunuzi wa mali. |
| **SIFA ZA UPENDELEO** | | |
| 6. | **Sifa za Upendeleo** | 6.1. Mtu au kampuni itakuwa na sifa za kufaidika na mpango wa upendeleo wa kitaifa ikiwa mtu huyo au kampuni inakidhi vigezo vilivyoainishwa hapa chini; -<br><br>Makampuni binafsi: -<br>a) Yatapaswa kusajiliwa katika Jamhuri ya Muungano na kuwa na yafuatayo:<br>i. Namba ya usajili wa Kampuni;<br>ii. Vyeti vya usajili wa Kampuni;<br>iii. Leseni za Biashara;<br>iv. Leseni za Sekta mahsusi, pale inapofaa<br>v. Cheti cha Udhibitisho wa kulipa Kodi; na<br>vi. Vibali, pale inapohitajika, vilivyotolewa na mamlaka husika kwa ajili ya shughuli zake.<br><br>b) Sehemu kubwa ya hisa za mtaji zilizolipwa za kampuni zinamilikiwa aidha na Serikali au na wananchi wa Tanzania. Muundo wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | umiliki wa hisa za kampuni binafsi unapaswa kuthibitishwa kupitia fomu za marejesho ya mwaka au taarifa za fedha zilizokaguliwa zilizowasilishwa kwa msajili wa kampuni kuthibitisha iwapo sehemu kubwa ya hisa zilizolipwa inayomilikiwa na Serikali au wananchi wa Tanzania; na<br><br>c) Kwamba hakuna utaratibu wowote wa sehemu kubwa ya faida halisi au manufaa mengine ya kampuni za ndani yatakayo ongezeka au kulipwa kwa watu ambao si raia wa Tanzania au kwa makampuni ambayo hayajakidhi vigezo vya upendeleo. Mambo yafuatayo yatapaswa kupitiwa:<br>i. Makubaliano ya mgawanyo wa faida, mikataba, na taratibu zozote nyingine kuhakikisha uzingatiwaji wa masharti;<br>ii. Sera za ugawaji wa gawio ili kuthibitisha kama sehemu kubwa ya faida inabaki nchini; na<br>iii. Taarifa kuhusu Tamko la manufaa ya umiliki wa kampuni.<br><br>(2) Kwa Ushirika wa kampuni za ndani;-<br><br>a) kampuni binafsi zilizosajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano;<br><br>b) sehemu kubwa ya mtaji wa hisa zilizolipwa za kampuni binafsi inayomilikiwa na raia wa Tanzania; |

| | | |
|---|---|---|
| | | c) Ushirika huo umesajiliwa na Mamlaka husika ndani ya Tanzania; na<br><br>d) Mtu binafsi hana utaratibu wowote wa sehemu kubwa ya faida halisi au manufaa mengine yatakayo ongezeka au kulipwa kwa watu ambao si raia wa Tanzania au kwa makampuni ambayo hayajakidhi vigezo vya upendeleo.<br><br>(3) Kwa wabia au watu binafsi wanaofanya biashara kama wakandarasi au washauri elekezi, sehemu kubwa ya hisa inamilikiwa na raia wa Tanzania. Taasisi Nunuzi inapaswa kupitia:<br><br>a) Nakili ya Mkataba wa Ubia kutoka kwa Msajili inayothibitisha umiliki na iwapo sehemu kubwa ya hisa zinamilikiwa na raia wa Tanzania;<br>b) Utambuzi wa mtu binafsi kupitia kitambulisho cha taifa au namba ya kitambulisho ili kuthibitisha utambulisho wa wamiliki;<br>c) Vyeti vya Usajili wa Biashara;<br>d) Leseni za Biashara;<br>e) Leseni za Sekta Mahsusi;<br>f) Vibali vilivyotolewa na Mamlaka husika kwa ajili ya shughuli zake; na<br>g) Leseni ya Uzingatiaji wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi<br><br>6.2 Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha 6.1 (2) (c), Ushirika utapaswa kuwa na yafuatayo, |

| | | |
|---|---|---|
| | | a) Barua ya kusudio au idhini kutoka kwa mamlaka husika kadri itakavyohitajika, kwa ajili ya kuunda Ushirika ikiambatana na rasimu ya makubaliano au makubaliano ya ushirika inayoainisha majukumu na wajibu wa kila upande pamoja na utaratibu wa mgawanyo wa faida au wajibu;<br><br>b) Usajili wa ushirika uliopo kutoka kwa mamlaka zinazohusika pale inapobidi;na<br><br>c) Makampuni binafsi yanayounda Ushirika yanapaswa kusajiliwa binafsi na mamlaka husika kama ilivyoainishwa katika kifungu kidogo 6.1 (1) (a) |
| **MPANGO WA UPENDELEO NA UKOMO** | | |
| 7. | **Upendeleo wa kitaifa** | 7.1. Taasisi nunuzi itapaswa, kutoa upendeleo wakati wa ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa kampuni za ndani au ushirika kati ya kampuni za ndani na kigeni na kwa bidhaa zilizotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br><br>7.2. Wazabuni ambao ni watu au kampuni za ndani au walio katika ushirika kati ya kampuni za ndani na za kigeni, watakuwa na sifa za kupewa upendeleo kama watatimiza vigezo vilivyoainishwa katika kifungu cha 6 cha Mwongozo huu.<br><br>7.3. Ukomo wa upendeleo utatolewa kama ifuatavyo;<br>a) Ukomo wa upendeleo utakuwa asilimia 10 kwa wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa ndani; |

| | | |
|---|---|---|
| | | b) Asilimia 8 kwa ushirika pale ambapo mchango wa wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa kigeni ni kati ya asilimia 26 hadi 49; na<br>c) Asilimia 10 kwa ushirika pale ambapo mchango wa wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa kigeni ni kati ya asilimia 0 – 25.<br>7.4. Nyaraka za zabuni zinapaswa kuonyesha wazi upendeleo na njia itakayotumika katika tathmini na ulinganisho wa zabuni ili kutekeleza upendeleo huo.<br>7.5. Baada ya zabuni kupokelewa na kufanyiwa mapitio na Taasisi Nunuzi, zabuni zilizokidhi vigezo vya tathmini zitagawanywa katika makundi yafuatayo:<br><br>a) Kundi A: Zabuni zinazowasilishwa na wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa ndani;<br><br>b) Kundi B: Zabuni zinazowasilishwa na ushirika wa ndani na wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa kigeni wanaokidhi vigezo vilivyoainishwa katika kifungu cha 6 cha Mwongozo huu; au<br><br>c) Kundi C: Zabuni zinazowasilishwa na wakandarasi, watoa huduma au washauri elekezi wa kigeni.<br><br>7.6. Taasisi Nunuzi itafanya mapitio ya taarifa za umiliki zilizowasilishwa pamoja na taarifa nyingine zinazohitajika ili kubaini iwapo muuzaji wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | bidhaa/mkandarasi au kundi la wauzaji bidhaa/wakandarasi wanastahili kupata upendeleo.<br>7.7. Taasisi nunuzi itatathmini na kulinganisha kwanza zabuni zote zinazokidhi vigezo ili kubaini zabuni yenye bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini ndani ya kila kundi.<br><br>7.8. Zabuni zenye bei ya chini zaidi zilizofanyiwa tathmini katika kila kundi zitalinganishwa na ikiwa, kutokana na ulinganisho huo, zabuni kutoka Kundi A au Kundi B ni ya chini zaidi, itachaguliwa kwa ajili ya tuzo ya mkataba.<br><br>7.9. Endapo zabuni kutoka Kundi C ndiyo zabuni yenye bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini, zabuni zote kutoka Kundi C zitalinganishwa zaidi na zabuni yenye bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini kutoka Kundi A na B.<br><br>(a) Kiasi sawa na ukomo maalum wa upendeleo kwa Kundi A kitaongezwa katika bei ya zabuni zilizopokelewa kutoka kwa mzabuni katika Kundi C; na<br><br>(b) Kiasi sawa na tofauti kati ya ukomo wa upendeleo wa kundi A na kundi B kitaongezwa katika bei ya zabuni iliyopokelewa kutoka kwa mzabuni katika kundi B.<br><br>7.10. Endapo zabuni kutoka katika Kundi A au B itakuwa yenye bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini, |

| | | |
|---|---|---|
| | | itachaguliwa kwa ajili ya tuzo ya mkataba. Endapo haijachaguliwa, zabuni yenye bei ya chini zaidi iliyofanyiwa tathmini kutoka Kundi C, itachaguliwa. |
| 8. | **Upendeleo wa Kipekee kwa watu na kampuni za ndani** | 8.1. Ununuzi wa kazi za ujenzi, bidhaa au huduma zenye thamani isiyozidi kiasi cha shilingi 50,000,000,000, utahifadhiwa kwa ajili ya watu au kampuni za ndani pekee.<br><br>8.2. Kampuni ya kigeni inaweza kushiriki katika zabuni zilizotengwa kwa upendeleo wa kipekee ikiwa tu itaunda Ushirika na kampuni ya ndani, ambapo mchango wa kampuni ya ndani katika ushirika ni asilimia 75. Pale ambapo Taasisi Nunuzi inapokea ofa moja tu inayokubalika kutoka kwa mtu au kampuni ya ndani dhidi ya ununuzi uliotengwa kwa upendeleo wa kimkoa, Taasisi Nunuzi inaweza kuzingatia kutoa tuzo kwa mtu au kampuni hiyo.<br><br>8.3. Pale ambapo mkataba wa ununuzi uliokusudiwa awali kwa kampuni za ndani, lakini hakuna ofa zinazokubalika zilizopokelewa, tuzo ya zabuni inaweza kutolewa kwa mzabuni wa kigeni ambaye atapaswa kuingia mkataba mdogo na kampuni ya ndani kwa kiasi kisichozidi asilimia 30 na kisichopungua asilimia 5 ya jumla ya thamani ya mkataba.<br><br>8.4. Katika matumizi ya upendeleo wa pekee kwa wauzaji wa bidhaa wa ndani, wakandarasi, washauri elekezi au watoa huduma, Taasisi Nunuzi itahakikisha kuwa mtu au kampuni iliyochaguliwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | inakidhi vigezo vya sifa vilivyotolewa chini ya kifungu cha 6 cha Mwongozo huu. |
| 9. | **Upendeleo wa Bidhaa za Ndani** | 9.1. Taasisi nunuzi itatoa upendeleo wa asilimia 15 kwa bidhaa zinazotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano na huduma zinazohusiana kwa mikataba iliyotolewa tuzo kwa misingi ya zabuni za ushindani wa kimataifa au kitaifa.<br><br>9.2. Taasisi Nunuzi itabainisha katika nyaraka ya zabuni maelekezo kwa muuzaji wa bidhaa kutoa kipaumbele kwa bidhaa zinazotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano.<br><br>9.3. Taasisi Nunuzi itabainisha katika nyaraka ya zabuni na mkataba kwa kazi za ujenzi na huduma, kutoa kipaumbele kwa kununua bidhaa zinazotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wakati wa utekelezaji wa mkataba.<br><br>9.4. Orodha ya bidhaa zinazotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano itakuwa kama ilivyotangazwa na PPRA katika Mfumo wa Kielectroniki wa Ununuzi wa Umma Tanzania (NeST).<br><br>9.5. Iwapo Taasisi Nunuzi itanunua bidhaa ambazo hazijatengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyoorodheshwa kwenye orodha iliyochapishwa na PPRA, ndani ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | siku tano za kazi baada ya kutolewa kwa tuzo ya mkataba, itawasilisha taarifa kwa Mamlaka ikieleza sababu za kutonunua bidhaa zilizotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano.<br><br>9.6. Kwa madhumuni ya kutoa upendeleo kwa bidhaa za ndani, Zabuni zitagawanywa katika makundi matatu kama ifuatavyo:<br><br>a) **Kundi A:** Zabuni zinazotoa bidhaa zilizotengenezwa, kuchimbwa au kuzalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano, ambazo:<br><br>i) Nguvu kazi, malighafi, na vifaa vyenye chanzo ndani ya Jamhuri ya Muungano na vinazaidi ya asilimia thelathini (30%) ya bei za bidhaa hizo zikiwa kiwandani; na<br><br>ii) Kituo cha uzalishaji ambacho bidhaa hizo zitatengenezwa, kuunganishwa au kuchakatwa kinapaswa kuwa kimejihusisha na utengenezaji, uunganishaji au uchakataji wa bidhaa hizo angalau tangu wakati cha kuwasilisha zabuni.<br><br>b) **Kundi B:** Zabuni nyingine zote zinazotoa bidhaa zinazotengenezwa ndani ya Jamhuri ya Muungano, ambazo nguvu kazi, malighafi na vifaa vyenye asili ya Jamhuri ya Muungano vinachangia chini ya asilimia thelathini (30%) ya bei za bidhaa hizo zikiwa kiwandani. |

| | | |
|---|---|---|
| | | c) **Kundi C:** Zabuni zinazotoa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinapaswa kuagizwa moja kwa moja.<br><br>9.7. Tathmini ya zabuni itafanyika kulingana na kifungu cha 36.2 cha Mwongozo huu |
| 10. | **Upendeleo wa Kimkoa** | 10.1. Upendeleo wa Kimkoa utajumuisha upendeleo kwa Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ndani ya mkoa.<br>10.2. Wakati wa utekelezaji wa upendeleo wa kimkoa, kipaumbele kitatolewa kwa wauzaji wa bidhaa, wakandarasi au watoa huduma wa ndani ambao wapo ndani ya vijiji, kata, halmashauri, na mikoa yao husika.<br>10.3. Upendeleo wa kimkoa kwa wauzaji wa bidhaa, wakandarasi, au watoa huduma wa ndani utatumika kwa zabuni ambazo thamani zake ni;<br>a) Kazi za ujenzi hadi Tshs 1,000,000,000.00<br>b) Bidhaa hadi Tshs 200,000,000.00;<br>c) Huduma zisizo za ushauri elekezi hadi Tshs 200,000,000.00; na<br>d) Huduma za Ushauri elekezi hadi Tshs 200,000,000.00<br>10.4. Pale ambapo Taasisi Nunuzi inapokea ofa moja tu inayokubalika kutoka kwa mtu au kampuni ya ndani dhidi ya ununuzi uliotengwa kwa upendeleo wa kimkoa, Taasisi Nunuzi inaweza kuzingatia kutoa tuzo kwa mtu au kampuni hiyo.<br>10.5. Pale ambapo Taasisi Nunuzi haijapokea zabuni zinazokubalika kutoka kwa watu au kampuni za ndani ya mkoa na ikiwa mahitaji ya zabuni bado |

| | | |
|---|---|---|
| | | yako halali, zabuni mpya zinaweza kuombwa kwa msingi usio na vizuizi.<br>10.6. Taasisi nunuzi zitatumia njia za ununuzi zinazofaa ambazo zinazingatia vigezo vya upendeleo wa kimkoa vilivyoainishwa katika Kifungu cha 10.3 cha Mwongozo huu.<br>10.7. Matumizi ya njia ya ununuzi ya kotesheni shindani (kotesheni ya kitaifa) kwa bidhaa, huduma zisizo za ushauri elekezi, na kazi za ujenzi, yatazuiliwa kwa mkoa isipokuwa tu thamani ya ununuzi hauzidi ukomo wa upendeleo wa kimkoa kama vilivyobainishwa katika Kifungu cha 10.3 cha Mwongozo huu. |
| **USHIRIKA, MKATABA MDOGO NA UBIA** | | |
| **A: USHIRIKA** | | |
| 11. | **Matumizi ya Ushirika** | 11.1. Sehemu A kuhusu Ushirika itatumika kwa zabuni zote zilizo chini ya upendeleo wa kipekee na zabuni zilizotengwa kwa ajili ya kujengea uwezo wazabuni wa ndani, na haitatumika kwa Ushirika ulioundwa katika zabuni zenye ukomo wa zaidi ya Tshs 50,000,000,000.00.<br>11.2. Kampuni au watu wa ndani wanaweza kuunda Ushirika na kampuni au watu wengine wa ndani kwa madhumuni ya kushiriki katika zabuni zilizotengwa mahsusi kwa kampuni au watu wa ndani kwa ajili ya kujenga uwezo.<br>11.3. Iwapo Ushirika ulioundwa kati ya kampuni au watu wa ndani hauna uwezo wa kushiriki katika zabuni zilizohifadhiwa kwa ajili ya kujenga uwezo, Ushirika |

| | | |
|---|---|---|
| | | wao unaweza kuingia katika Ushirika na kampuni ya kigeni kwa madhumuni ya kujenga uwezo.<br><br>11.4. Uundwaji wa Ushirika kati ya kampuni za ndani na kampuni ya kigeni, mchango wa kampuni ya ndani katika ushirika hautakuwa chini ya asilimia sabini na tano (75%) na kampuni ya ndani itakuwa kampuni kiongozi katika zabuni hiyo. |
| 12. | **Uundwaji wa Ushirika** | 12.1. Wazabuni wanaokusudia kushiriki katika zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi, huduma za ushauri elekezi na huduma zisizo za ushauri elekezi wanaweza kuunda Ushirika kwa madhumuni ya kuongeza uwezo na ushindani katika zabuni.<br><br>12.2. Ushirika unaweza kuundwa kati ya kampuni mbili au zaidi za ndani pekee, au kati ya kampuni ya ndani au za ndani au Ushirika wa ndani na kampuni za kigeni.<br>12.3. Wahusika katika Ushirika wanaweza kuchangia mtaji, nguvu kazi, Mali, ujuzi, uzoefu, maarifa, au rasilimali nyingine zinazofaa kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba au mradi.<br><br>12.4. Ili kustahili kushiriki katika mchakato wa zabuni za bidhaa, kazi za ujenzi, huduma za ushauri elekezi na huduma zisizo za ushauri elekezi au kupewa tuzo ya mkataba, ushirika wowote ulioanzishwa inapaswa kusajiliwa ndani ya Tanzania na mamlaka kadri inavyohitajika.<br><br>12.5. Kampuni ya ndani inayounda sehemu ya Ushirika itasajiliwa ndani ya Tanzania, na sehemu kubwa ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | hisa ya mtaji iliyolipwa kwa kampuni ya ndani itamilikiwa na Serikali au raia wa Tanzania. Aidha, hakuna taratibu zozote ambazo sehemu kubwa ya faida kamili au Faida nyingine zitakayopatikana zitalipwa kwa watu ambao si raia wa Tanzania au kampuni za kigeni, au kuhamishwa katika akaunti za nje ya nchi.<br><br>12.6. Kampuni ya ndani itawasilisha katika zabuni yake, ushahidi wa sifa zake kama ulivyobainishwa chini ya kifungu cha 6 cha Mwongozo huu.<br>12.7. Wahusika katika ushirika wataingia kwenye makubaliano ya Ushirika katika muundo ulioainishwa kwenye Kiambatisho cha 4 na 5 cha Mwongozo huu, na watabainisha kati ya mambo mengine, haki, wajibu, majukumu, na mgawanyo wa rasilimali za kifedha kwa kila mhusika katika Ushirika.<br><br>12.8. Makubaliano ya Ushirika yatakuwa sehemu ya mkataba wa ununuzi kati ya Taasisi ya Ununuzi na Ushirika.<br><br>12.9. Uvunjwaji wa masharti na vigezo vya Ushirika na upande wowote wa Ushirika unaweza kusababisha kusitishwa kwa mkataba wa ununuzi au hatua nyingine za kisheria ikiwemo kufungiwa kwa Ushirika na Wakurugenzi wake. |
| 13. | **Mahitaji ya Ushirika** | 13.1. Pale ambapo Ushirika unaundwa kati ya kampuni ya ndani na kampuni ya kigeni kwa madhumuni ya kuwa na sifa za kupata upendeleo wa kitaifa, angalau asilimia 51 ya hisa za mtaji zilizolipwa za |

| | | |
|---|---|---|
| | | kampuni ya ndani zinapaswa kumilikiwa na Serikali au raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<br>13.2. Katika Ushirika kati ya kampuni ya ndani na kampuni ya kigeni, kampuni ya ndani itatoa katika mkataba au mradi si chini ya asilimia 50 ya wafanyakazi muhimu wanaohitajika kwa utekelezaji wa mkataba au mradi.<br>13.3. Makubaliano ya Ushirika yataeleza vyeo vya wafanyakazi muhimu watakaochangia kwa kila muhusika katika Ushirika.<br><br>13.4. Mchango wa rasilimali za kifedha za kampuni ya ndani kwenye Ushirika hautakuwa chini ya asilimia 50 ya rasilimali za kifedha zinazohitajika kutekeleza mkataba.<br><br>13.5. Ugawaji wa faida kutoka kwenye mkataba wa ununuzi uliotolewa kwa ushirika unaweza pia kufuata kiasi cha mchango wa kifedha wa wahusika katika Ushirika. |
| 14. | **Kuwasilisha zabuni kwa Ushirika** | 14.1. Pale ambapo Ushirika umeruhusiwa katika mchakato wa zabuni, Taasisi Nunuzi itaeleza hitaji hilo katika Nyaraka ya zabuni.<br><br>14.2. Zabuni zilizowasilishwa zitajumuisha barua ya nia au barua ya idhini kutoka kwa mamlaka husika ya usajili wa Ushirika na rasimu ya makubaliano ya Ushirika au makubaliano ya Ushirika yaliyosainiwa na wahusika wote katika ushirika. Uwasilishaji wa zabuni na mawasiliano yote ya Ushirika yatakuwa kwa jina la ushirika kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya Ushirika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 14.3. Makubaliano ya Ushirika yatabainisha mhusika kiongozi katika Ushirika ambaye atawawakilisha wahusika wengine wakati wa mchakato wa zabuni na utekelezaji wa mkataba. |
| 15. | **Wajibu dhidi ya Ushirika** | 15.1. Kampuni zinazoshiriki katika Ushirika zitawajibika kwa pamoja na binafsi kwa Taasisi Nunuzi. |
| **UINGIAJI MKATABA MDOGO** | | |
| 16. | **Mahitaji ya Uingiaji Mkataba Mdogo** | 16.1. Pale ambapo mkataba wa ununuzi uliokusudiwa kwa kampuni za ndani lakini hakuna ofa iliyopokelewa imekubalika, zabuni inaweza kutolewa kwa mkandarasi wa nje ambaye atapaswa kuingia mkataba mdogo na kampuni ya ndani kwa asilimia isiyozidi 30 na isiyopungua asilimia 5 ya jumla ya thamani ya mkataba.<br>16.2. Kwa mujibu wa kifungu cha 16.1, bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zitakazofanywa kwa mkataba mdogo hazitajumuisha Makisio ya Gharama na Gharama Kuu.<br>16.3. Katika utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha 16.1, Taasisi nunuzi itaeleza katika nyaraka za zabuni hitaji la kampuni ya kigeni kuingia mkataba mdogo katika sehemu ya mkataba mkuu na kampuni ya ndani.<br>16.4. Taasisi nunuzi itamtaka mzabuni wa kigeni kubainisha katika zabuni yake asilimia na aina ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma atakazoingia mkataba mdogo na kampuni ya ndani. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 16.5. Pale inapotokea uingiaji wa mkataba mdogo wa ndani, mzabuni wa kigeni atapaswa kubainisha katika zabuni yake moja ya yafuatayo:<br>a) Sehemu ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma atakazoingia mkataba mdogo na kampuni ya ndani na kutoa maelezo ya kampuni ya ndani atakayoingia nayo mkataba ndogo, kwa kujaza "Fomu ya Nia ya Kuingia mkataba mdogo" katika muundo uliobainishwa katika jedwali la Mwongozo huu;<br><br>b) Sehemu ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma atakazoingia mkataba mdogo bila kubainisha kampuni ya ndani atakayoingia nayo mkataba mdogo, na mzabuni wa kigeni atapata kampuni ya ndani kwa taratibu zake binafsi baada ya kupewa tuzo ya mkataba na kabla ya kusaini mkataba; au<br><br>c) Sehemu ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma atakazoingia mkataba mdogo bila kubainisha kampuni ya ndani atakayoingia nayo mkataba mdogo, na mzabuni wa kigeni anaweza kubainisha kuwa kampuni ya ndani itapatikana kwa usaidizi wa Taasisi nunuzi, na kampuni ya kigeni itawajibika kwa kampuni ya ndani atakayoingia nayo mkataba mdogo itakayopatikana kwa utaratibu huo<br>16.6. Ikiwa ni mkataba mdogo ulioteuliwa, Taasisi nunuzi itashirikisha kampuni ya ndani kuwa mkandarasi mdogo kupitia mchakato wa ununuzi wa ushindani |

| | | |
|---|---|---|
| | | na kuagiza kampuni ya nje kufanya kazi na mkandarasi mdogo aliyeteuliwa.<br><br>Kwa madhumuni ya kifungu hiki:<br><br>"Kuingia mkataba mdogo wa ndani" maana yake ni njia ya kuingia mkataba mdogo ambapo mzabuni anachagua mkandarasi mdogo wa kushirikiana naye; na<br><br>“Uingiaji mkataba mdogo ulioteuliwa" maana yake ni njia ya kuingia mkataba mdogo ambapo Taasisi nunuzi inashirikisha kampuni ya ndani kuwa mkandarasi mdogo kupitia mchakato wa ununuzi wa ushindani na kukubaliana na kampuni ya kigeni kufanya kazi za ujenzi na mkandarasi mdogo alieteuliwa. |
| 17. | **Utaratibu wa kuingia Mkataba mdogo ulioteuliwa** | 17.1. Taasisi nunuzi, Kwa madhumuni ya kuingia mkataba mdogo ulioteuliwa, itatumia mchakato wa ushindani kubaini wakandarasi wadogo watakaoteuliwa kupewa tuzo ya mkataba mdogo.<br>17.2. Taasisi nunuzi itaandaa wigo wa kazi tofauti na bili ya makadirio ya ujenzi kwa ajili ya mkandarasi mkuu na mkandarasi mdogo, na haitaalika zabuni zenye bei kwa wakandarasi wadogo kabla ya mkandarasi mkuu kupewa tuzo wa mkataba.<br>17.3. Zabuni yenye mkataba mdogo itaidhinishwa na Afisa Masuuli au Bodi ya Zabuni, kadiri itakavyokuwa, bila kujali ni mkandarasi mkuu au Taasisi nunuzi iliyoalika zabuni.<br>17.4. Zabuni zitaalikwa kwa jina la mkandarasi mkuu ambaye anaweza kushauriwa kuhusu taratibu |

| | | |
|---|---|---|
| | | zozote mahususi anazotaka kujumuisha katika nyaraka za zabuni ya mkataba mdogo.<br>17.5. Zabuni iliyochaguliwa na Taasisi nunuzi itawasilishwa kwanza mkandarasi mkuu kwanza kwa mapitio kabla maelekezo ya kuikubali kama mkataba mdogo kutolewa.<br>17.6. Taasisi nunuzi itahitaji mkandarasi mkuu kuongeza wigo wa kazi, bidhaa au huduma kutoka mkataba mkuu kwenda mkataba mdogo ili kukidhi ukomo ikiwa thamani ya mkataba mdogo haitakidhi ukomo uliobainishwa wakati wa mchakato wa zabuni.<br>17.7. Wigo wa kazi au huduma zilizoongezwa chini ya kifungu kidogo cha 17.6 zitatumia viwango vya malipo katika zabuni za mkataba mdogo kwa kuweka bei, ambapo vigezo msawazo na mahitaji vinalinganishwa kwa zingatia maelezo na vipimo vya kazi au huduma.<br>17.8. Taasisi nunuzi, pale ambapo wigo wa kazi za ujenzi, bidhaa au huduma zilizoongezwa hazilingani na wigo wa kazi ya mkandarasi mdogo, itatumia viwango vya malipo vya mkataba mkuu kuweka bei ya kazi zilizoongezwa. |
| 18. | **Utaratibu wa kuingia mkataba mdogo na mkandarasi wa Ndani** | 18.1. Mkandarasi Mkuu atateua kampuni ya ndani ya chaguo lake ambayo inakidhi vigezo kulingana na kifungu cha 6 cha Mwongozo huu kushiriki katika ununuzi wa umma kuwa mkandarasi mdogo.<br>18.2. Mkandarasi mkuu atapaswa, kwa madhumuni ya kuingia mkataba mdogo na mkandarasi wa ndani |

| | | |
|---|---|---|
| | | chini ya kifungu cha 16.6 cha Mwongozo huu, atajumuisha yafuatayo katika zabuni yake:<br><br>a) Maelezo yanayohusiana na asilimia na wigo wa kazi ya ujenzi au huduma zitakazoingiwa mkataba mdogo;<br><br>b) Nyaraka zinazoonyesha uthibitisho wa vigezo na sifa za mkandarasi mdogo iwapo mkandarasi mdogo ametambuliwa; na<br><br>c) Barua ya kusudio ya kuingia mkataba mdogo na makubaliano ya kuingia mkataba mdogo uliopendekezwa ikiwa upo. |
| 19. | ***Utaratibu wa Tathmini*** | 19.1. Wakati wa tathmini, Taasisi nunuzi itatoa ukomo wa upendeleo wa hadi asilimia 6% kwa kampuni ya kigeni ambayo inaingia mkataba mdogo wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa kampuni ya ndani kulingana na ukomo ulioanishwa hapa chini:<br>a) Upendeleo wa asilimia 6 utapaswa kutolewa wakati thamani ya mkataba mdogo uliopendekezwa kuingiwa ni kati ya asilimia 23 na 30 ya bei ya zabuni;<br><br>b) Upendeleo wa asilimia 4 utapaswa kutolewa wakati thamani ya mkataba mdogo uliopendekezwa kuingiwa ni kati ya asilimia 16 na 22 ya bei ya zabuni;<br><br>c) Upendeleo wa asilimia 2 utapaswa kutolewa wakati thamani ya mkataba mdogo |

| | | |
|---|---|---|
| | | uliopendekezwa kuingiwa ni kati ya asilimia 10 na 15 ya bei ya zabuni; na<br><br>d) Upendeleo wa asilimia 1 utapaswa kutolewa wakati thamani ya mkataba mdogo uliopendekezwa kuingiwa ni kati ya asilimia 5 na 9 ya bei ya zabuni.<br><br>19.2. Mzabuni aliyetathminiwa kuwa na bei ya chini zaidi katika zabuni ya mkataba mdogo atateuliwa na Taasisi nunuzi kuwa mkandarasi mdogo<br><br>19.3. Mkandarasi mdogo aliyeteuliwa ataingia kwenye makubaliano ya mkataba mdogo na mkandarasi mkuu. |
| 20. | **Makubaliano ya Mkataba mdogo** | 20.1. Makubaliano yoyote yaliyoingiwa kati ya kampuni ya kigeni na mkandarasi mdogo yatakuwa sehemu ya mkataba mkuu kati ya Taasisi Nunuzi na kampuni ya kigeni.<br><br>20.2. Iwapo kampuni ya kigeni itasitisha makubaliano na mkandarasi mdogo, Taasisi Nunuzi itahakikisha kampuni ya ndani yenye sifa zinazofanana au zaidi inachukua nafasi ya mkandarasi mdogo wa awali. |
| 21. | **Usimamizi wa Mikataba Midogo** | 21.1. Mkandarasi mdogo aliyeteuliwa atakuwa chini ya usimamizi wa mkandarasi mkuu, na vihatarishi vinavyohusiana na mkataba mdogo vitabebwa na mkandarasi mkuu.<br><br>21.2. Mkandarasi mdogo chini ya mkataba mdogo wa ndani uliongiwa atakuwa chini ya usimamizi, |

| | | |
|---|---|---|
| | | uangalizi na uratibu wa mkandarasi mkuu, na vihatarishi vinavyohusiana na mkataba mdogo zitabebwa na mkandarasi mkuu.<br><br>21.3. Malipo kwa bidhaa, kazi au huduma zilizothibitishwa kutekelezwa na mkandarasi mdogo yatalipwa moja kwa moja na Taasisi Nunuzi kwenye akaunti ya benki ya mkandarasi mdogo. |
| 22. | **Uundaji wa Ushirika au mkataba mdogo na Kampuni za kigeni** | 22.1. Taasisi nunuzi itahakikisha kuwa, kampuni zote za kigeni zinazoshiriki katika zabuni ambazo ukomo wake ni juu ya Tshs. 50,000,000,000.00 zinashiriki katika mchakato wa ununuzi kama ushirika na kampuni ya ndani au kuingia mkataba mdogo wa sehemu ya mkataba na kampuni ya ndani baada ya kupewa mkataba wa ununuzi.<br><br>22.2. Taasisi Nunuzi itabainisha katika nyaraka ya zabuni husika iwapo zabuni mahususi inaruhusu uundwaji wa ushirika au uingiaji wa mkataba mdogo.<br><br>22.3. Ikiwa ni Ushirika, kampuni ya kigeni na ya ndani zitakubaliana kuhusu vigezo na masharti ya ushirika.<br><br>22.4. Ikiwa ni uingiaji wa mkataba mdogo, kampuni ya kigeni itatoa mkataba mdogo kwa kampuni ya ndani kati ya asilimia 5 – 30 ya bei ya mkataba.<br><br>22.5. Makubaliano ya ushirika yatakuwa sehemu ya mkataba wa ununuzi utakaoingiwa kati ya Taasisi nunuzi na Ushirika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 22.6. Uvunjifu wa vigezo na masharti ya ushirika au mkataba mdogo na upande wowote inaweza kusababisha kusitishwa kwa mkataba wa ununuzi au hatua nyingine za kisheria ikijumuisha kufungiwa kwa ushirika na wakurugenzi wake. |
| **C: UBIA** | | |
| 23. | **Uundaji wa Ubia** | 23.1. Wazabuni wanaweza kuunda Ubia kwa madhumuni ya kupata upendeleo maalum<br><br>23.2. Ubia unaweza kuundwa kati ya kampuni/watu wa ndani au kati ya kampuni/watu wa ndani na wa kigeni.<br><br>23.3. Ikiwa Ubia utaundwa kati ya kampuni/watu wa ndani na kampuni/watu wa kigeni, Ubia huo hautapata upendeleo maalum isipokuwa kampuni ya ndani inamiliki angalau asilimia 51 (51%) ya hisa za mtaji zilizolipwa (mchango wa wabia) katika Ubia. |
| 24. | **Uthibitisho wa Umiliki wa Hisa** | 24.1. Kwa Ubia unaojumuisha kampuni za ndani na za kigeni, wakati wa zabuni, kampuni ya ndani itawasilisha Nakili ya Mkataba wa Ubia kutoka kwa Msajili wa Majina ya Biashara inayoonyesha kuwa inamiliki hisa za mtaji zilizolipwa kama ilivyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha 23.3 cha Mwongozo huu.<br><br>24.2. Kampuni ya ndani ambayo itashindwa kutoa uthibitisho huo itajinyima yenyewe haki ya upendeleo maalum. |

| | | |
|---|---|---|
| 25. | **Mchango wa Rasilimali** | 25.1. Kila makubaliano ya ubia yataeleza wazi mchango wa rasilimali watu, mtaji na majukumu ya washirika.<br><br>25.2. Kampuni/mtu wa ndani atachangia angalau asilimia 50 ya wafanyakazi muhimu wanaohitajika kutekeleza mkataba.<br><br>25.3. Mchango wa rasilimali za kifedha za mzabuni wa ndani kwenye Ubia hautakuwa chini ya asilimia 50 ya rasilimali za kifedha zinazohitajika kutekeleza mkataba.<br><br>25.4. Ugawaji wa faida kutoka kwenye mkataba wa ununuzi uliotolewa kwa Ubia unaweza kufuata pia kiasi cha mchango wa kifedha wa pande zote za Ubia. |
| 26. | **Upendeleo kwa Wabia** | 26.1. Wakati wa tathmini, kwa mujibu wa vifungu 23, 24 na 25 vya Mwongozo huu, Taasisi nunuzi itatoa upendeleo wa asilimia 10 kwa kampuni ya kigeni inayounda Ubia na kampuni ya ndani katika ununuzi wa kazi za ujenzi, bidhaa, au huduma. |
| **USHIRIKI WA WAZABUNI WA KIGENI KATIKA HUDUMA ZA USHAURI ELEKEZI** | | |
| 27. | **Ujumuishaji wa wataalamu na kampuni za ndani katika huduma za ushauri elekezi** | 27.1. Isipokuwa chini ya ununuzi wa dharura, mshauri elekezi wa kigeni anayeshiriki katika zabuni yoyote ya huduma za ushauri elekezi atajumuisha katika zabuni yake wataalamu au kampuni za ndani.<br><br>27.2. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 27.1 cha Mwongozo huu, ujumuishaji wa wataalamu au kampuni za ndani utatumika kwa zabuni zote zilizo au zisizo chini ya mpango wa upendeleo. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 27.3. Taasisi nunuzi itaainisha katika mwaliko wa zabuni masharti ya kujumuishaji wataalamu au kampuni za ndani katika zabuni na idadi ya chini ya wataalamu wa ndani wataojumuishwa katika mkataba wa ushauri elekezi haitakuwa chini ya asilimia 50 ya wafanyakazi muhimu. Ujumuishaji wa wataalamu wa ndani na mshauri elekezi wa kigeni katika zabuni yake utathibitishwa kwa kuwasilisha nakala ya vyeti vya elimu na kitaaluma vilivyohakikiwa na wasifu uliosainiwa wa wataalamu wa ndani kama ilivyoainishwa katika nyaraka ya zabuni.<br><br>27.4. Ukomo wa upendeleo kwa zabuni za kiufundi utakuwa kama ilivyotolewa chini ya kifungu kidogo 7.3 cha Mwongozo huu.<br><br>27.5. Katika uzito wa alama ya kifedha uliotengwa, alama tano (5) zitatengwa kwa ajili ya kukokotoa alama ya kifedha kwa mujibu wa uwiano wa fedha zilizotengwa kwa kampuni ya kigeni na ya ndani.<br><br>27.6. Ukomo wa upendeleo kwa zabuni za kifedha utatathminiwa kama ifuatavyo:<br>(a) Baada ya zabuni ya kifedha ya kampuni zilizofuzu kufunguliwa na kufanyiwa mapitio na kamati ya tathmini, zabuni zilizokidhi zitagawanywa katika makundi yafuatayo:<br><br>**Kundi A**: zabuni za kifedha zilizotolewa na washauri elekezi wa ndani na muungano kati ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | washauri elekezi wa ndani, wanaostahili kupewa upendeleo;<br><br>**Kundi B:** zabuni za kifedha zilizowasilishwa kwa muungano kati ya washauri elekezi wa ndani na kigeni, wanaostahili kupewa upendeleo; na<br><br>**Kundi C:** zabuni za kifedha zilizowasilishwa na washauri elekezi wa kigeni.<br><br>(b) Kwa madhumuni ya tathmini na ulinganifu wa zabuni za kifedha:<br><br>(i) Ukomo wa upendeleo uliobainishwa utaongezwa kwa **Kundi A**;<br>(ii) Ukomo wa upendeleo uliobainishwa utakokotolewa kulingana na uwiano wa fedha uliotengwa kwa kampuni za ndani kwa **Kundi B**; na<br>(iii) Ukomo wa upendeleo uliobainishwa hautagawiwa kwa **Kundi C**.<br><br>27.7. Ukokotoaji kwa ajili ya tathmini na kulinganishaji wa zabuni za kifedha chini ya mpango wa upendeleo utakuwa kama ilivyoelezwa kwenye **kiambatisho cha 6** cha Mwongozo huu.<br><br>27.8. Mzabuni wa kigeni ambaye atashindwa kujumuisha katika zabuni yake wataalamu wa ndani kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo 27.3, atajumuisha katika zabuni yake ushahidi kutoka kwa vyombo vya kitaaluma vilivyowekwa kisheria nchini |

| | | |
|---|---|---|
| | | Tanzania kuthibitisha kuwa wafanyakazi muhimu wa ndani wanaohitajika hawapatikani nchini Tanzania. |
| 28. | **Uundaji wa Ushirika au Muungano katika mikataba ya ushauri elekezi** | 28.1. Kwa mujibu wa kifungu 27.1, ujumuishaji wa kampuni za ndani na mshauri elekezi wa kigeni katika huduma za ushauri elekezi utafanywa kwa kuunda Ushirika au muungano na kampuni ya ndani.<br><br>28.2. Pale ambapo Ushirika au Muungano utaundwa kati ya kampuni ya kigeni na kampuni ya ndani, kampuni ya ndani itapaswa kumilikiwa kwa asilimia 100 na raia wa Tanzania.<br><br>28.3. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 6.1, kampuni ya ndani itawasilisha katika zabuni yake, ushahidi wa usajili wake nchini Tanzania na nakala ya fomu iliyokamilishwa iliyotolewa na BRELA inayothibitisha kiasi cha hisa za mtaji kilicholipwa na kampuni ya ndani.<br><br>28.4. Katika Ushirika au Muungano kati ya kampuni ya ndani na kampuni ya kigeni, kila upande wa Ushirika utatenga kwenye mkataba au mradi asilimia 50 ya wafanyakazi muhimu wanaohitajika kutekeleza mkataba au mradi.<br><br>28.5. Wahusika katika ushirika au muungano wataingia katika Makubaliano ya Ushirika katika muundo uliowekwa katika Jedwali la Kwanza la Mwongozo huu na watabainisha haki, wajibu, majukumu, na ugawanyaji wa rasilimali za kifedha kwa kila sehemu ya Ushirika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 28.6. Makubaliano ya Ushirika au Muungano utaainisha vyeo vya wafanyakazi muhimu watakaojumuishwa katika mkataba au mradi na kila upande wa Ushirika.<br><br>28.7. Mchango wa rasilimali za kifedha wa kampuni ya ndani kwa Ushirika au Muungano hautakuwa chini ya asilimia 50 ya rasilimali za kifedha zinazohitajika kutekeleza mkataba.<br><br>28.8. Makubaliano wa ushirika au muungano utakuwa sehemu ya mkataba wa ununuzi utakaoingiwa kati ya Taasisi Nunuzi na Ushirika au Muungano.<br><br>28.9. Uvunjaji wa vigezo na masharti vya Ushirika au Muungano na upande wowote kunaweza kusababisha kusitishwa kwa mkataba wa ununuzi au kuchukuliwa hatua nyingine za kisheria ikijumuisha kufungiwa kwa Ushirika au Muungano na Wakurugenzi wake. |
| **KUJENGA UWEZO KWA WATU AU KAMPUNI ZA NDANI** | | |
| 29. | **Utengaji wa zabuni kwa ajili ya kujenga Uwezo** | 29.1. Taasisi Nunuzi zitatenga si chini ya asilimia 30 ya Mpango wao wa Ununuzi wa Mwaka kwa ajili ya zabuni kwa watu au makampuni ya ndani.<br><br>29.2. Idara tumizi kwa kushirikiana na Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi itapaswa kubainisha katika Taarifa yake ya Mahitaji, zabuni zitakazotengwa kwa ajili ya watu au kampuni za ndani kabla ya kuwasilishwa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi.<br><br>29.3. Taasisi Nunuzi itaainisha katika Mpango wa Ununuzi wa Mwaka zabuni zilizotengwa chini ya mipango |

| | | |
|---|---|---|
| | | mbalimbali ya upendeleo kwa kuchagua upendeleo mahususi utakaotumika katika kila zabuni.<br><br>29.4. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 29.1, Taasisi Nunuzi itatoa sababu za kushindwa kwake kutenga asilimia 30 ya Mpango wake wa ununuzi mwaka kwa ajili ya mpango wa upendeleo na sababu zilizotajwa, pamoja na Mpango wa Ununuzi wa Mwaka utawasilishwa kwa mamlaka ya uidhinishaji bajeti kwa ajili ya idhini.<br><br>29.5. Taasisi nunuzi itaandaa taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa kifungu cha 29 cha Mwongozo huu katika muundo uliowekwa chini ya Jedwali la Nne la Mwongozo huu na kuiwasilisha kwa Mamlaka.<br><br>29.6. Taasisi nunuzi inaruhusiwa kugawanya zabuni kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo wazabuni wa ndani.<br><br>29.7. Taasisi nunuzi itaruhusu uundaji wa Ushirika katika nyaraka za zabuni katika zabuni zote zilizotengwa kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa wazabuni wa ndani. |
| 30. | **Mazingatio ya Wastani wa Mauzo kwa Mwaka** | 30.1. Fomyula ya kukokotoa Wastani wa Mauzo ya Mwaka (WMM)ni kama ulivyotolewa hapa chini: -<br><br>WMM= jumla ya Mauzo ya Mwaka gawanya kwa idadi ya miaka<br>*Kwa mfano; -*<br>*Bei ya zabuni: bilioni 15* |

| | | |
|---|---|---|
| | | *Dhani, Mauzo M 1= 11,000,000,000*<br>*M2 = 13,000,000,000*<br>*M3 = 15,000,000,000*<br>*Makadirio ya mauzo ya mwaka kwa kipindi: Miaka Mitatu (3)*<br>*Wastani wa mauzo ya mwaka*<br>*= (M1+ M2+ M3)/3*<br>*=39,000,000,000/3*<br>*WMM= 13,000,000,000*<br><br>30.2. Wastani wa mauzo ya mwaka ya mzabuni kwa kipindi cha muda flani hayapaswi kuwa chini ya asilimia 50 ya bei yake ya zabuni.<br><br>Kwa mfano uliopo chini ya kifungu kidogo cha 30.2 cha Mwongozo huu, mauzo ya kila mwaka ya mzabuni lazima yawe sawa na au zaidi ya 1/4 x 15 bilioni = 3.75 bilioni.<br>Utaratibu wa kukokotoa wastani wa mauzo wa mwaka umetolewa katika Kiambatisho cha 7 cha Mwongozo huu. |
| 31. | **Uzoefu wa kuzingatiwa kwa Makampuni ya Ndani** | 31.1. Katika zabuni za kazi za ujenzi na huduma, ambapo Taasisi Nunuzi inahitaji wazabuni kuwasilisha uthibitisho wa uzoefu wa jumla na/au tamko la uzingatiwaji wa masuala ya ukatili, unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia, uzoefu unaoendana/mahsusi, ikiwa ni kwa kampuni za ndani ambazo hazina uzoefu, kigezo hiki kitaondolewa na badala yake tathmini itafanywa kuhusiana na: -<br><br>a) Sifa na uzoefu wa wafanyakazi muhimu; |

| | | |
|---|---|---|
| | | b) Ubora na idadi ya vifaa muhimu vilivyopendekezwa (pale inapohitajika)<br>c) Ubora wa mbinu za kukamilisha kazi;<br>d) Uelewa wa hadidu za rejea za kazi (pale inapohitajika);<br>e) Historia ya Mashauri ya kimahakama;<br>f) kipindi cha kukamilisha kazi;<br>g) Tamko la uzingatiwaji wa masuala ya ukatili, unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia;<br>h) Uhalali wa Zabuni;<br>i) Hati ya Uwakilishi Kisheria;<br>j) Upatikanaji wa Fedha/ mikopo, na<br>k) Vigezo vingine kulingana na aina ya kazi:<br><br>i) Mpango wa usimamizi wa Vihatarishi;<br><br>ii) Mkakati wa ukusanyaji wa vifaa;<br><br>iii) Mpango wa eneo la kazi;<br><br>iv) mkakati wa usimamizi wa ujenzi;<br><br>v) Ratiba ya Maandalizi ya kazi;<br><br>vi) Mkakati na Mpango wa Utekelezaji Usimamizi wa Mazingira na jamii; na<br><br>vii) Mpango wa Usimamizi wa Usalama na Afya.<br><br>31.2. Utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha 31.1 utatumika tu kwa zabuni zenye thamani isiyozidi ukomo wa upendeleo wa kipekee wa kikanda. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 31.3. Ikiwa ni ununuzi wa zabuni za kazi za ujenzi, masharti ya kifungu kidogo cha 31.1 yatatumika kwa wakandarasi wa Daraja la VI au VII. |
| **MASHARTI YA JUMLA** | | |
| 32. | **Ushiriki wa wazabuni wa kigeni katika zabuni awali zilizotengwa kwa ajili ya wazabuni wa ndani** | 32.1. Zabuni yoyote iliyo ndani ya ukomo wa upendeleo wa kipekee haitakuwa wazi kwa wazabuni wa kigeni.<br><br>32.2. Bila ya kujali masharti ya kifungu ndogo cha 32.1, pale ambapo Taasisi Nunuzi haijapata wazabuni wa ndani kwa zabuni zilizotangazwa chini upendeleo wa kipekee, wazabuni wa kigeni wanaweza kualikwa kushiriki katika zabuni hiyo.<br><br>32.3. Wazabuni wa kigeni wanaoshiriki katika zabuni chini ya kifungu hiki watashiriki katika mchakato wa zabuni kama Ushirika na kampuni ya ndani au kwa kuingia mkataba mdogo wa sehemu ya kazi au huduma kwa kampuni za ndani kwa kutumia taratibu zilizoainishwa katika Mwongozo huu. |
| 33. | **Ajira kwa mfanyakazi msaidizi wa ndani** | 33.1. Katika mkataba wowote wa kazi za ujenzi, bidhaa, ushauri elekezi au huduma zisizo za ushauri elekezi, Taasisi nunuzi itaeleza katika nyaraka za zabuni aina au kundi la wafanyakazi wasaidizi wa ndani ambao wataajiriwa na mkandarasi, muuzaji bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa kigeni kusaidia utekelezaji wa mkataba. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 33.2. Mkandarasi, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa kigeni atawasilisha katika zabuni yake, kundi na idadi ya wafanyakazi wasaidizi wa ndani ambao watahusika katika utekelezaji wa mkataba na muda wa usaidizi huo utatolewa.<br><br>33.3. Wakati wa utekelezaji wa mkataba, Taasisi nunuzi itahakikisha mkandarasi, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa kigeni aliyepewa mkataba wa ununuzi anaajiri wafanyakazi wasaidizi wa ndani.<br><br>33.4. Mfanyikazi msaidizi wa ndani atabadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na mfanyakazi msaidizi wa ndani mwenye sifa sawa na zaidi.<br><br>33.5. Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo katika mahitaji ya mwajiri, mkandarasi atafanya utaratibu wa kushirikisha wafanyakazi na vibarua wote, wa ndani au vinginevyo, na kwa malipo, makazi, chakula na usafiri wao. |
| 34. | **Upendeleo kwa kampuni za ndani zinazounda ushirika na Kampuni nyingine za Ndani** | 34.1. Katika zabuni za kazi za ujenzi zilizotengwa kwa ajili ya upendeleo wa kipekee kwa makampuni ya ndani, mkandarasi aliye na daraja la juu la usajili (Daraja la kwanza na la pili) anaweza kuingia katika Ushirika na mkandarasi aliye na daraja la chini la usajili (daraja la tatu hadi la saba) kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo.<br><br>34.2. Kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 34.1, Ushirika utakaoundwa utapewa ukomo wa upendeleo kama ifuatavyo |

| | | |
|---|---|---|
| | | a) Pale ambapo mchango wa mkandarasi aliye na daraja la juu la usajili na ule wa mkandarasi aliye na kiwango cha chini cha usajili ni asilimia 50 kwa kila mmoja, Ushirika utapewa upendeleo wa asilimia 15;<br>b) Pale ambapo mchango wa mkandarasi aliye na daraja la chini la usajili ni kati ya asilimiaa 26 hadi 49 ya thamani ya mkataba, Ushirika utapewa upendeleo wa asilimia 10; na<br>c) Pale ambapo mchango wa mkandarasi mwenye daraja la chini la usajili ni kati ya asilimia 1 hadi 25 ya thamani ya mkataba, Ushirika utapewa ukomo wa upendeleo wa asilimia 6.<br><br>34.3. Nyaraka ya zabuni itajumuisha masharti kwamba kwa mkandarasi aliye na daraja la juu la usajili (Daraja la I na daraja la II) anaweza kuingia katika Ushirika na mkandarasi aliye na daraja la chini la usajili (Daraja la III hadi Daraja la VII).<br><br>34.4. Tathmini ya zabuni itafanywa kwa mujibu wa Kifungu cha 36.2 cha Mwongozo huu. |
| 35. | **Upendeleo kwa makampuni ya ndani yanayoingia mkataba mdogo wa kazi za ujenzi na makampuni mengine ya ndani** | 35.1. Katika zabuni za kazi za ujenzi zilizotengwa kwa ajili ya upendeleo wa kipekee kwa makampuni ya ndani, mkandarasi aliye na daraja la juu la usajili (Daraja la I na Daraja la II) anaweza kuingia mkataba mdogo wa sehemu ya kazi za ujenzi na mkandarasi mwenye daraja la chini la usajili (Daraja la III hadi Daraja la VII) kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 35.2. Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 35.1, uingiaji wa mkataba mdogo utapewa ukomo wa upendeleo kama ifuatavyo:<br>a) Pale ambapo mkandarasi mwenye Daraja la juu la usajili anapoingia mkataba mdogo kati ya asilimia 20 hadi 30 ya kazi za ujenzi na mkandarasi mwenye daraja la chini la usajili, mkandarasi mwenye daraja la juu la usajili atapewa ukomo wa upendeleo wa asilimia 10;<br><br>b) Pale ambapo mkandarasi mwenye Daraja la juu la usajili anapoingia mkataba mdogo kati ya asilimia 10 hadi 19 ya kazi za ujenzi na mkandarasi mwenye daraja la chini la usajili, mkandarasi mwenye daraja la juu la usajili atapewa ukomo wa upendeleo wa asilimia 8; na<br><br>c) pale ambapo mkandarasi mwenye Daraja la juu la usajili anapoingia mkataba mdogo kati ya asilimia 1 hadi 9 ya kazi za ujenzi na mkandarasi mwenye daraja la chini la usajili, mkandarasi mwenye daraja la juu la usajili atapewa ukomo wa upendeleo wa asilimia 5.<br><br>35.3. Nyaraka ya zabuni itajumuisha masharti kwamba kwa mkandarasi aliye na daraja la juu la usajili (Daraja la I na daraja la II) anaweza kuingia katika mkataba mdogo na mkandarasi aliye na daraja la chini la usajili (Daraja la III hadi Daraja la VII).<br><br>35.4. Tathmini ya zabuni itafanywa kwa mujibu wa Kifungu 36.2 cha Mwongozo huu. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 35.5. Mkataba mdogo utaingiwa kwa kufuata taratibu zilizoelezwa katika kifungu cha 16 cha Mwongozo huu.<br><br>35.6. Malipo ya kazi za ujenzi au huduma zilizothibitishwa zinazotekelezwa na mkandarasi mdogo yatalipwa moja kwa moja na Taasisi nunuzi kwenye akaunti ya benki ya mkandarasi mdogo. |
| 36. | **Ukomo wa Upendeleo kwa Wauuzaji wa bidhaa, Washauri elekezi na watoa huduma zisizo za ushauri elekezi wa ndani wanaoingia mkataba mdogo na Wauuzaji wa bidhaa, Washauri elekezi na watoa huduma zisizo za ushauri elekezi wa ndani** | 36.1. Katika zabuni za bidhaa, Huduma za ushauri elekezi na zisizo za ushauri elekezi zilizotengwa kwa ajili ya upendeleo wa kipekee kwa makampuni ya ndani ukomo wa Upendeleo kwa muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara za kati au kubwa kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Kitaifa ya Biashara Ndogo na za Kati, 2003 (kama ilivyorekebishwa) Uingiaji mkataba mdogo na muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara ndogo ndogo au ndogo kama ilivyoainishwa na Sera kwa zabuni chini ya Upendeleo wa Kipekee.<br><br>36.2. Ukomo wa upendeleo utatolewa kwa kampuni ya ndani inayoingia mkataba mdogo kama ifuatavyo: -<br><br>a) Pale ambapo muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara za kati au kubwa anaingia mkataba mdogo kati ya asilimia 20 hadi 30 ambaye mtaji wake wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | uwekezaji uko katika kundi la biashara ndogo ndogo au ndogo, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani katika kundi la biashara za kati au kubwa atapewa ukomo upendeleo wa asilimia 10;<br><br>b) Pale ambapo muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara za kati au kubwa anaingia mkataba mdogo kati ya asilimia 10 hadi 19 ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara ndogo ndogo au ndogo, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani katika kundi la biashara za kati au kubwa atapewa ukomo upendeleo wa asilimia 8; na<br><br>c) Pale ambapo muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara za kati au kubwa anaingia mkataba mdogo kati ya asilimia 1 hadi 9 ambaye mtaji wake wa uwekezaji uko katika kundi la biashara ndogo ndogo au ndogo, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mshauri elekezi wa ndani katika kundi la biashara za kati au kubwa atapewa ukomo upendeleo wa asilimia 5.<br><br>36.3. Malipo ya kazi za ujenzi au huduma zilizothibitishwa zinazotekelezwa na mkandarasi mdogo yatalipwa moja kwa moja na Taasisi nunuzi kwenye akaunti ya benki ya mkandarasi mdogo. |

| | | |
|---|---|---|
| 37. | **Upendeleo kwa kampuni mama za ndani** | 37.1. Kwa mujibu wa vifungu vya 34, 35, 36 na 37 ukomo wa upendeleo hautatolewa kwa kampuni mama zinazounda ushirika au zinazoingia mkataba mdogo na kampuni zake tanzu.<br><br>37.2. Kwa mujibu wa vifungu vya 34, 35, 36 na 37, ukiukaji wa vigezo na masharti ya Ushirika au mkataba mdogo na upande wowote utasababisha kusitishwa kwa mkataba wa ununuzi au chukuliwa hatua nyingine za kisheria ikijumuisha kufungiwa kwa ushirika na wakurugenzi wake. |
| 38. | **Malipo kwa kampuni za ndani** | 38.1. Taasisi nunuzi, kabla ya kuanzisha mchakato wa ununuzi chini ya mpango wa upendeleo, itahakikisha kuwa fedha za utekelezaji wa mkataba zimetengwa na kuidhinishwa.<br><br>38.2. Taasisi Nunuzi itahakikisha kwamba malipo kwa wazabuni wa ndani yanafanywa ndani ya muda kulingana na masharti ya malipo yaliyoainishwa katika nyaraka za mkataba. |
| 39. | **Tathmini ya zabuni chini ya mipango ya upendeleo** | 39.1. Katika tathmini ya zabuni zilizotengwa kwa ajili ya kujenga uwezo ambazo zimewasilishwa kwa muundo wa ubia au Ushirika, vigezo kuhusu uzoefu, mtiririko wa fedha, mauzo ya mwaka, wafanyakazi muhimu, na thamani ya miradi iliyotekelezwa vitaunganishwa na havitatathminiwa kwa mtu binafsi au kampuni.<br><br>39.2. Tathmini ya zabuni chini ya mpango wa upendeleo itafanywa kwa taratibu zilizoainishwa katika: |

| | | |
|---|---|---|
| | | a) Mwongozo wa Tathmini ya Bidhaa, Kazi za ujenzi na Huduma zisizo za Ushauri elekezi, 2024; na<br>b) Mwongozo wa Tathmini wa Huduma za Ushauri, 2024. |
| 40. | **Mafunzo kwa wahitimu wanaojifunza kwa Vitendo** | 40.1. Kwa madhumuni ya kujenga uwezo wa wahitimu wanaojifunza kwa Vitendo wakati wa utekelezaji wa mikataba ya kazi za ujenzi/huduma za ushauri elekezi na zisizo za ushauri elekezi, Taasisi nunuzi itaainisha katika zabuni yake mahitaji ya wahitimu watakaohusika kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na kubainisha maeneo ya kujengewa uwezo kama ifuatavyo: -<br><br>a) Kwa miradi ya kazi za ujenzi ambayo ukomo wake ni chini ya Shilingi za kitanzania bilioni moja ya Tanzania, si chini ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo watatu (3);<br><br>b) Kwa miradi ya kazi za ujenzi ambayo ukomo wake ni zaidi ya Shilingi za kitanzania bilioni moja ya Tanzania, si chini ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo watano (5);<br><br>c) Kwa mradi wa kazi za ujenzi unahusisha kampuni ya nje, si chini ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo kumi (10);<br><br>d) Kwa huduma za ushauri elekezi, si chini ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo wawili (2); na |

| | | |
|---|---|---|
| | | e) Kwa huduma zisizo za ushauri elekezi pale inapohitajika, mtoa huduma atatoa nafasi kwa ajili ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo wasio pungua wawili (2).<br><br>40.2. Kwa madhumuni ya kujenga uwezo wahitimu wanaojifunza kwa vitendo wakati wa utekelezaji wa mikataba, Taasisi nunuzi itaainisha katika nyaraka zake za zabuni idadi ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo na maeneo ya kujengewa uwezo.<br><br>40.3. Taasisi nunuzi itaainisha katika nyaraka za zabuni chanzo cha wahitimu wanaojifunza kwa vitendo kutoka katika mpango wa serikali wa wahitimu wanaojifunza kwa vitendo ambao wataambatishwa katika utekelezaji wa mradi/kazi.<br><br>40.4. Kwa mujibu wa kifungu cha 41.2, vyanzo vya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo vitajumuisha Mamlaka ya Huduma za Ajira Tanzania (TAESA), Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), na taasisi nyingine yoyote husika na vyombo vya kitaalamu.<br><br>40.5. Taasisi Nunuzi itaomba wahitimu wanaojifunza kwa vitendo kutoka Taasisi, Wakala na vyombo vya Kitaalamu husika kwa ajili ya kuwekwa kwenye mradi/kazi maalum kwa kuzingatia wafanyakazi muhimu waliohitajika katika utekelezaji wa mradi/kazi husika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 40.6. Taasisi, Wakala na vyombo vya kitaaluma husika vitatoa kwa Taasisi Nunuzi wigo wa mafunzo kwa wahitimu wanaojifunza kwa vitendo waliowekwa katika utekelezaji wa mkataba.<br><br>40.7. Taasisi Nunuzi itaeleza katika nyaraka za zabuni kiasi cha jumla kwa ajili wa wahitimu wanaojifunza kwa vitendo kwa kuzingatia kima cha chini cha mshahara kwa idadi ya wahitimu wanaojifunza kwa vitendo inayohitajika kwa mujibu wa Mwongozo huu.<br><br>40.8. Wahitimu wanaojifunza kwa vitendo walioambatishwa katika mradi/kazi mahususi wataandaa taarifa za kila mwezi zitakazowasilishwa kwa meneja wa mkataba, Taasisi, Wakala na vyombo vya Kitaaluma. |
| 41. | **Utatuzi wa Migogoro** | 41.1. Mgogoro wowote utakaojitokeza kutokana na utekelezaji wa Mwongozo huu utafuata taratibu za utatuzi wa migogoro zilizoainishwa katika nyaraka za zabuni, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni zake. |
| 42. | **Ufuatiliaji wa Mwongozo huu** | 42.1. Mamlaka itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa upendeleo kwa Taasisi nunuzi. |
| 43. | **Mapitio ya Mwongozo** | 43.1. Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu, au pale itakapohitajika, au pale itakapo lazimu. |

**VIAMBATISHO**

## VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Fomu ya Taarifa za Wanachama wa Ushirika

**Mzabuni atajaza fomu hii kuzingatia maelekezo yaliyoainishwa hapa chini. Jedwali lifuatalo litajazwa na mzabuni na kwa kila Mwanachama wa Ushirika**

Tarehe: [weka tarehe (siku, mwezi na Mwaka) ya uwasilishaji wa zabuni

Namba ya RFB: [weka namba ya mchakato wa zabuni]

**N**amba Mbadala: [weka namba ya utambulisho ikiwa ni zabuni mbadala]

| |
|---|
| 1. Jina la Mzabuni: [weka jina la kisheria la Mzabuni] |
| 2. Jina la Mwanachama wa Ushirika: [weka jina la kisheria la Mwanachama la Ushirika] |
| 3. Nchi ya Usajili ya Mzabuni Mwanachama wa Ushirika: [weka nchi ya usajili wa Mwanachama wa Ushirika] |
| 4. Mwaka wa Usajili wa Mzabuni Mwanachama wa Ushirika: [weka mwaka wa usajili wa Mwanachama wa Ushirika] |
| 5. Anwani ya rasmi ya Mzabuni Mwanachama wa ushirika katika nchi ya usajili: [weka anwani ya Mwanachama katika nchi ya usajili] |
| 6. Taarifa za Mwakilishi wa Mzabuni Mwanachama wa Ushirika alieidhinishwa<br>**Jina:** [weka jina la mwakilishi wa mwanachama wa ushirika aliyeidhinishwa]<br>**Anwani:** [weka anwani ya mwakilishi wa mwanachama wa ushirika aliyeidhinishwa]<br>**Namba za Simu/Faksi:** [weka namba za simu/faksi za mwakilishi wa mwanachama wa ushirika aliyeidhinishwa]<br>**Anwani ya Barua pepe:** [weka barua pepe ya mwakilishi wa mwanachama wa ushirika aliyeidhinishwa] |

7. Viambatisho ni nakala za nyaraka halisi za [weka tiki kwenye boksi la nyaraka halisi zilizoambatishwa]

☐ Hati za Usajili (au sawa na nyaraka za katiba au muungano), na/au hati za usajili wa kampuni iliyotajwa hapo juu, kulingana na ITB 4.4.

☐ Ikiwa ni kampuni au taasisi inayomilikiwa na serikali, Nyaraka za uthibitisho wa uhuru wa kisheria na kifedha, uendeshaji kulingana na sheria za biashara, na kwamba hazipo chini ya usimamizi wa mwajiri, kulingana na Mwongozo huu].

8. Muundo wa Taasisi, orodha ya Bodi ya Wakurugenzi, na wanafaika wa umiliki vimeambatishwa. [Mzabuni mshindi atatoa taarifa za ziada kuhusu manufaa ya umiliki kwa kila mwanachama wa ushirika kwa kutumia Fomu ya kubainisha wanufaika wa Umiliki].

Kiambatisho 2: Fomu ya Kubainishwa Wanafaika wa Umiliki.

**MAELEKEZO KWA WAZABUNI: FUTA KISANDUKU HIKI BAADA YA KUJAZA FOMU**

*Fomu hii ya* kubainisha wanufaika wa Umiliki *("Fomu") inajazwa na Mzabuni mshindi. Ikiwa ni ushirika, Mzabuni atawasilisha fomu tofauti kwa kila mwanachama. Maelezo ya wanufaika wa umiliki yatakayowasilishwa katika fomu hii yatatambuliwa kuwa ndio maelezo halisi kwa tarehe yaliyowasilishwa.*

Kwa madhumuni ya fomu hii, mnufaika wa umiliki wa Mzabuni ni mtu yeyote ambaye anamiliki au anamdhibiti mzabuni kwa kukidhi moja au zaidi ya masharti yafuatayo:

- *Anashikilia moja moja kwa moja au kutoshikilia moja kwa moja asilimia 25 au zaidi ya hisa*
- *Anashikilia moja kwa moja au kutoshikilia moja kwa moja asilimia 25 au zaidi ya haki za kupiga kura*
- *Ana haki ya moja kwa moja au kutokuwa na haki ya moja kwa moja ya kuteua idadi kubwa ya Wakurugenzi wa bodi au sawa na bodi ya Usimamizi wa mzabuni*

Kiambatisho 3: Tamko la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamii

**Tamko la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamii**

Tarehe: [*weka siku, Mwezi, Mwaka]*

Namba na jina la Mkataba: [*weka Namba na jina ya Mkataba*

Kwa:

[weka jina la Mwajiri/Mteja/Mnunuzi] (chagua inayofaa)

[*Weka Anwani kamili ya Mwajiri/Mteja/Mnunuzi] (Chagua inayofaa)*

Tamko:

Mimi/Sisi, tuliosaini hapa chini, tunatamka kama ifuatavyo:

1. Uelewa wa Wajibu

Mimi/Sisi tunatambua kuwa chini ya vigezo na masharti ya mkataba uliotajwa hapo juu, nina/tuna wajibu wa kuhakikisha uzingatiaji kwa uhaminifu wa dhamana ya uhifadhi mazingira na jamii na [Mkandarasi/Muuzaji/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi] (chagua inayofaa) kuhusiana na wajibu wote chini ya mkataba.

2. Matokeo ya Kutotekeleza

Mimi/Sisi tunakubali kwamba endapo tutashindwa kutekeleza mkataba kwa mujibu wa vigezo na masharti vya kimazingira na jamii viliyowekwa, Mimi/Sisi tunaweza kufungiwa kushiriki katika ununuzi wa umma kwa muda utakaobainishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni zake.

3. Uhalali wa Tamko

Tamko hili la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na litakuwa halali hadi hapo kazi itakapotekelezwa kikamilifu na kukubaliwa rasmi na Mwajiri/Mteja/Mnunuzi (chagua linalofaa).

Limetolewa na kusainiwa na:

*Jina: [weka jina la mtu anayesaini Tamko la dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamii*

*Sahihi: [weka sahihi ya mtu ambaye jina na wadhifa wake umeonyeshwa]*

*Cheo: [ weka wadhifa wa kisheria wa mtu anayesaini Tamko dhamana la Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira na jamii]*

Imeidhinishwa kusaini Mkataba kwa niaba ya: [weka jina kamili la Mkandarasi/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi/Muuzaji wa Bidhaa] (chagua inayofaa).

*Imesainiwa leo ….. siku ya ….., ….. [weka tarehe ya kusaini]*

Gonga Muhuri wa Kampuni (kama inavyopaswa)

Kiambatisho 4: Fomu ya Mfano ya Makubaliano ya Ushirika – Kampuni na mtu wa ndani

**MAKUBALIANO YA USHIRIKA**

MAKUBALIANO HAYA YA USHIRIKA (hapa yataitwa “Makubaliano”) yameingiwa tarehe …………. siku ya mwezi wa ……… 20…… na kati ya:

[Jina na anwani ya kampuni/mtu wa ndani] (hapa ataitwa “[Jina Fupi au Kifupisho]”), ambapo litajumuisha warithi wake, wawakilishi wa kisheria na walioteuliwa kwa mujibu wa sheria, ambaye kwa madhumuni ya Makubaliano haya ataitwa “Mwanachama”;

NA

[Jina na anwani ya kampuni/mtu wa ndani] (hapa ataitwa “[Jina Fupi au Kifupisho]”), ambapo litajumuisha warithi wake, wawakilishi wa kisheria na walioteuliwa kwa mujibu wa sheria, ambaye kwa madhumuni ya Makubaliano haya ataitwa “Mwanachama”;

NA (idadi ya kadri watakavyoruhusiwa katika nyaraka za zabuni)

“Wanachama wa Ushirika” hapo juu kwa madhumuni ya Makubaliano haya kila mmoja ataitwa “Mwanachama” na kwa pamoja wataitwa “Wanachama”.

JINA LA USHIRIKA ULIOUNDWA NA ANWANI

Wanachama wamekubaliana kuungana katika muundo wa Ushirika kwa jina la [Taja Jina la Ushirika].

NA KWAMBA;

(a) Mnunuzi/Mwajiri/Mteja (kama ilivyofafanuliwa hapa chini) anakusudia kuteua/amewateua [Muuzaji wa Bidhaa/Mkandarasi/Mtoa Huduma] kwa ajili ya kutoa [Taja Huduma husika iwe bidhaa/kazi za ujenzi/Huduma]; hapa itaitwa “Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma”; na

Wanachama wamekubaliana kuungana katika muundo Ushirika ili kutekeleza [Taja Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma].

**KWAHIYO SASA**, Wanachama wamekubaliana kama ifuatavyo:

## 1.0. MAANA ZA MANENO

Maneno na maelezo yafuatayo yatakuwa na maana yaliyopewa, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo:

“Mnunuzi”/“Mwajiri”/“Mteja” maana yake ni Taasisi Nunuzi iliyotajwa katika [jedwali la 1];

Nchi” maana yake ni nchi iliyotajwa katika [jedwali la 1] ambapo mkataba utatekelezwa

Mwaliko” maana yake ni mwaliko wa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kwa Mwanachama au Wanachama kuwasilisha zabuni ya [Bidhaa/Ujenzi/Huduma];

“Ushirika” maana yake ni muunganiko ulioundwa kati ya wazabuni wawili au zaidi kwa mujibu wa Makubaliano haya;

“Makubaliano ya Ushirika” hapa yatarejewa kama “Makubaliano haya”, yanajumuisha nyaraka yenye Vigezo na Masharti pamoja na Jedwali la kwanza hadi la nne yaliyoambatishwa na makubaliano haya, na nyaraka nyingine zozote zitakazoanishwa katika [jedwali la kwanza] kuwa sehemu ya Makubaliano haya.

“Mwanachama Kiongozi” maana yake ni mwanachama atakayeongoza usimamizi wa shughuli za Ushirika na atakayetoa Mwakilishi wa Ushirika kwa ajili ya mawasiliano;

Kamati ya Usimamizi wa Ushirika” maana yake ni kamati iliyoundwa na Wawakilishi wa Wanachama wa Ushirika yenye jukumu la kusimamia shughuli za Ushirika (kutunga sera na kuteua mwakilishi wa Ushirika);

Mradi” maana yake ni bidhaa/kazi za ujenzi/huduma zilizopendekezwa au halisi zilizotajwa katika [jedwali la kwanza] ambazo Mnunuzi/Mwajiri/Mteja anakusudia au ameanza kununua na anahitaji muuzaji wa bidhaa/mkandarasi/mtoa huduma.

“Zabuni” maana yake ni ofa, pendekezo au kotesheni iliyoandaliwa na kuwasilishwa na Ushirika kujibu Mwaliko

“Bidhaa”/“Kazi za ujezi”/“Huduma” maana yake ni bidhaa/kazi za ujenzi/huduma zote zitakazosambazwa/kujengwa/kutekelezwa na ushirika kwa mujibu wa masharti ya Zabuni na Mkataba utakaotokana na zabuni hiyo.

"Makubaliano ya Huduma” maana yake ni makubaliano kati ya Mteja na Ushirika kwa ajili ya kutoa huduma za kitaalamu kwa Mradi;

Meneja wa Mkataba” maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Kamati ya Usimamizi wa Ushirika kusimamia mkataba wa bidhaa/kazi za ujenzi/huduma kwa mujibu wa Kifungu Kidogo 7.12.

2.0. USHIRIKA

2.1. Wanachama hapa wanaanzisha Ushirika uliojumuisha muungano usiorasmi kwa jina la [*jina la Ushirika*] au jina jingine watakalokubaliwa kwa muda husika (hapa utaitwa “Ushirika”) kwa madhumuni ya:

i. *Kuandaa na kuwasilisha zabuni kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja;*
ii. Kutoa taarifa ya yoyote ya ziada, Mnunuzi/Mwajiri/Mteja anaweza kuhitaji au kufanya majadiliano na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kuhusu masuala yeyote yanayohitaji majadiliano kuhusiana na zabuni;
iii. Kuingia mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja iwapo zabuni inakubaliwa; na
iv. Kusambaza bidhaa/kujenga/kutoa huduma zote chini ya mkataba wa Usambazaji/Kazi za ujenzi/ huduma.

2.2. Hivyo basi Wanachama wanamteua Mwanachama Kiongozi ambaye atakuwa mwakilishi wa Ushirika, na atathibitisha anwani ya Ushirika na anwani za Wanachama husika kama ilivyoelezwa katika [jedwali kwanza].

2.3. Isipokuwa kama imekubaliwa vinginevyo kwa maandishi na Wanachama, Makubaliano haya hayatasitishwa iwapo Mwanachama atabadilisha jina lake au akichukuliwa na, au kuunganishwa na, kampuni nyingine au ubia, mradi tu jina, kampuni au ubia unaofuata uwe kampuni ya usambazaji/ujenzi/taaluma huru inayokubalika kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja

2.4. Mchango wa kila Mwanachama katika Ushirika utatolewa chini ya jedwali lifuatalo:

Jedwali: Mchango wa Ushirika

| **Na** | **Aina ya Mchango kwa Ushirika** | **Mwanachama 1 (%)** | **Mwanacham a 2(%)** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Kifedha | | |
| 2. | Mchango wa wafanyakazi | | |

1.1. Baada ya utekelezwaji wa Makubaliano ya Ushirika, kila Mwanachama atatoa Hati ya Uwakilishi wa Kisheria ya mtu atakayemchagua kama Mwakilishi wake, kama ilivyoainishwa katika [jedwali la 1]

1.2. Wawakilishi wa Kila Mwanachama wataunda Kamati ya usimamizi wa Ushirika. Kupitia Hati ya Uwakilishi wa Kisheria iliyotolewa kwa wawakilishi, mwakilishi wa kila mwanachama atakuwa na mamlaka ya kusaini Makubaliano ya Ushirika kwa niaba ya kampuni yake

1.3. Mwanachama Kiongozi atateua Mwakilishi atakayewakilisha Ushirika katika mchakato wa ununuzi.

2.0. UWASILISHAJI WA ZABUNI

2.1. Wanachama watafanya jitihada zote zinazowezekana kupata tuzo ya zabuni ya Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma kutoka kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kwa mujibu wa

masharti ya Mwaliko au masharti yatakayokubaliwa baadae kati ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja na Ushirika.

2.2. Chini ya uratibu wa Mwanachama Kiongozi, wanachama kwa pamoja wataandaa na kuwasilisha zabuni kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja.

2.3. Wanachama watashirikiana na Mwanachama Kiongozi kutekeleza majukumu yao wanayostahili kwa ujuzi, uangalifu na umakini kama yalivyopangwa na kamati ya usimamizi wa Ushirika hadi kutolewa kwa tuzo na kusainiwa kwa Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma kwa ushirika, au hadi masharti ya Kifungu cha 16 yatakapotimizwa

2.4. Mwanachama Kiongozi atatoa Hati ya Uwakilishi wa kisheria kwa mwakilishi wake ambaye atakuwa na mamlaka ya kuwasilisha zabuni na kusaini mkataba kwa niaba na kwa jina la Ushirika. Saini ya mwakilishi wa mwanachama kiongozi itaufunga Ushirika katika kutekeleza wajibu na majukumu yote yaliyopo chini ya Mkataba

2.5. Mara baada ya Zabuni kuwasilishwa kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja, hakuna mabadiliko yanayoweza kufanyika au kuongezwa taarifa za ziada au kutolewa kwa maelezo bila ridhaa ya Wanachama wote hadi pale Mkataba wa Usambazaji/kazi za ujenzi/Huduma utakapoanza kutekelezwa

2.6. Ushirika utapaswa kuingia katika mkataba wa Usambazaji/Kazi za ujenzi /Huduma na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja iwapo tuzo itatolewa kwa Ushirika.

## 3.0. WAJIBU WA USHIRIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MKATABA

3.1. Ushirika utatekeleza Mkataba wa bidhaa / kazi za ujenzi / huduma ulioingiwa kati ya Ushirika na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kwa mujibu wa vigezo na masharti ya mkataba na makubaliano hayo ya Ushirika. iwapo kutakuwa na utofauti wowote kati ya mkataba wa bidhaa/kazi za ujenzi/huduma na Makubaliano haya ya ushirika, mkataba wa bidhaa/kazi/huduma utatumika.

3.2. Kila Mwanachama atawajibika kutimiza majukumu yaliyoanishwa katika [jedwali la 2] kwa mujibu wa masharti ya Mkataba wa bidhaa/kazi za ujenzi/huduma kwa kumridhisha kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja.

3.3. Mgawanyo wa majukumu ya Ushirika kati ya Wanachama kwa mujibu wa [jedwali la 2] unaweza kurekebishwa kwa makubaliano kati ya Wanachama, baada ya kupata idhini ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja

3.4. Iwapo inahitajika, mabadiliko au nyongeza yoyote ya bidhaa/kazi za ujenzi/huduma zinazopaswa kusambazwa/kutekelezwa/kutolewa chini ya Mkataba wa bidhaa/kazi za ujenzi/huduma yatafanywa kwa ridhaa au maelekezo ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja. Wajibu wa kutekeleza majukumu ya ziada utakuwa kwa mujibu wa makubaliano baina ya wanachama.

## 4.0. LUGHA NA SHERIA

4.1. Makubaliano ya Ushirika yatakuwa kwa Lugha ya Kiingereza.

4.2. Makubaliano haya yataongozwa na Sheria za Tanzania.

## 5.0. UPEKEE

5.1. Isipokuwa kama Wanachama watakubaliana vinginevyo, hakuna Mwanachama atakayejihusisha na shughuli yoyote inayohusiana na Mradi, isipokuwa kama Mwanachama wa Ushirika kwa mujibu wa masharti na vigezo vya Makubaliano hayo. Kila Mwanachama anathibitisha kwamba kampuni tanzu na kampuni nyingine au watu binafsi ambao wapo chini ya udhibiti wa mwanachama watazingatia masharti.

## 6.0. MAMLAKA YA UTENDAJI

6.1. Hakuna Mwanachama atakayekuwa na mamlaka ya kufunga au kuweka ahadi yoyote kwa niaba ya Ushirika au Mwanachama mwingine yeyote isipokuwa mamlaka hayo yameelezwa kwa maandishi na Wanachama kwa pamoja kuhusu Ushirika, au na Mwanachama mmoja mmoja kuhusu Mwanachama mwingine.

6.2. Kutoka tarehe ya Makubaliano haya hadi utoaji wa tuzo ya Mkataba wa Bidhaa/kazi za ujenzi/Huduma kwa Ushirika au hadi Makubaliano haya yatakapositishwa kwa mujibu wa na masharti yake au lolote litakalotokea mapema zaidi, masuala yafuatayo yatahitaji idhini ya pamoja ya Wanachama:

- Kwa madhumuni ya kuwasilisha Zabuni, majukumu na wajibu husika utakaotekelezwa na Wanachama kulingana na masharti ya Mwaliko

- Kwa madhumuni ya kuwasilisha Zabuni, Vigezo na masharti vilivyojumuishwa katika Zabuni ambavyo kwa ujumla vinatumika katika ushirika, na kwa mwanachama mmoja mmoja, kwa mujibu wa masharti ya Mwaliko; na

- Mawasiliano yoyote kwa, au majibu ya mawasiliano kutoka, kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja, yakiwa katika maandishi au kwa njia ya mdomo na ahadi yoyote kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja au mtu mwingine yeyote kuhusiana na Zabuni.

6.3. Kuanzia tarehe ya tuzo ya Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma kwa Ushirika, maamuzi kuhusu sera za Ushirika yatakuwa chini ya Kamati ya usimamizi wa Ushirika inayojumuisha Wawakilishi wa kila Mwanachama waliobainishwa kulingana na Kifungu Kidogo cha 2.6.

6.4. Kila Mwanachama atatoa taarifa ya Mwakilishi wake katika Kamati ya usimamizi wa Ushirika kwa Mwanachama mwingine na atatoa taarifa mapema kuhusu mabadiliko yoyote ya uteuzi wa muda au vinginevyo, yanayoweza kutokea mara kwa mara;

6.5. Mwakilishi wa Mwanachama Kiongozi katika Kamati ya Usimamizi wa Ushirika atakuwa Mwenyekiti wa Kamati. Mwenyekiti ataitisha mikutano ya kawaida ya Kamati na anaweza kualika watu wengine ambao anataka wahudhurie kwa madhumuni ya kutoa taarifa, ushauri kwa wawakilishi, au kuweka kumbukumbu za mwenendo wa Kamati.

6.6. Iwapo itatokea kuto kubaliana kati ya Wanachama wa Kamati ya Usimamizi wa Ushirika kuhusu masuala ambayo hayajawekwa bayana katika Makubaliano haya, Mwenyekiti atakuwa na haki ya kutumia kura ya turufu;

6.7. Mikutano ya Kamati ya Usimamizi wa Ushirika itafanyika angalau [Weka Idadi ya Mikutano] isipokuwa Wanachama watakubaliana vinginevyo. Mwanachama anaweza kuitisha mkutano wa Kamati wakati wowote kwa kutoa angalau taarifa ya maandishi ya siku saba;

6.8. Muhtasari wa mikutano utakuwa kwa lugha ya Kiingereza na nakala za Muhtasari za mikutano ya Kamati ya Usimamizi zitasambazwa kwa Wanachama;

6.9. Wanachama kwa pamoja wanakubaliana kutenda (na kukubaliana kuwa Wawakilishi wao katika Kamati ya Usimamizi wa Ushirika wanatenda) kwa wakati wote kwa maslahi ya Ushirika katika kuchukua hatua zozote zinazohusiana na Mradi na watatumia jitihada za busara kutatua migogoro itakayojitokeza baina yao kuhusiana na Ushirika;

6.10. Isipokuwa Wanachama watakubaliana vinginevyo, Mwanachama Kiongozi atakuwa na mamlaka ya kuteua Meneja wa Mkataba, pia kumuondoa kutoka katoka nafasi hiyo na kumteua mwingine;

6.11. Ushirika utamjulisha kwa maandishi Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kuhusu uteuzi, uondoshwaji au mabadiliko ya Meneja wa Mkataba;

6.12. Meneja wa Mkataba atasimamia na kuongoza utekelezaji wa Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma kwa kuzingatia maelekezo ya Kamati ya Usimamizi wa Ushirika, na atatoa taarifa kwa Kamati ya Usimamizi wa Ushirika juu ya utekelezaji na maendeleo ya mkataba pale inapohitajika na Kamati hiyo;

6.13. Kila Mwanachama anaweza kuteua Mwakilishi katika eneo ambalo mwanachama atafanyia kazi. Mwakilishi atakuwa na wajibu wa kutekeleza majukumu ya Mwanachama wake katika eneo husika chini ya Mkataba huu;

6.14. Kila Mwanachama atamjulisha mwingine kuhusu Mwakilishi wake pamoja na majukumu aliyopewa, na atatoa taarifa mapema kuhusu mabadiliko yoyote ya uteuzi huo au mgao wa majukumu yanayoweza kujitokeza mara kwa mara;

6.15. Wawakilishi watafanya kazi chini ya usimamizi wa Meneja wa Mkataba.

## 7.0. NYARAKA

7.1. Nyaraka zote zinazotolewa na Mwanachama au Wanachama kuhusiana na Mradi na ambazo zinatolewa kwa watu wengine tofauti na Wanachama zitabeba jina la Ushirika

7.2. Nyaraka zote zilizoandaliwa na mmoja kati ya wanachama kuhusiana na utekelezaji wa Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma, na ambazo zinawasilishwa kwa mteja au kutolewa kwa watu wengine, zitasainiwa na Mwakilishi aliyeidhinishwa wa Mwanachama Kiongozi;

7.3. Kila Mwanachama atakuwa na haki ya kupata taarifa bila kikomo kuhusu shughuli yoyote ya mradi inayotekelezwa na Wanachama kuhusiana na Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma

7.4. Nakala za nyaraka zote zinazowasilishwa kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja na au kwa niaba ya Ushirika na Mwanachama, zitasambazwa kwa Wanachama wengine haraka kadri inavyowezekana mara baada ya kuwasilishwa huko;

7.5. Katika kipindi cha Makubaliano haya na baada ya kusitishwa kwa Makubaliano bila kikomo cha muda, Mwanachama yeyote hatapaswa kuweka wazi kwa mtu yeyote taarifa yoyote atakayopata kutokana na ushiriki wake katika Ushirika (na atahakikisha kuwa wafanyakazi wake pia wanazingatia masharti hayo) isipokuwa taarifa hiyo

- inajulikana kwa umma;
- Inapaswa kuwekwa wazi kwa ajili ya usahihi wa usambazaji/ujenzi/utendaji wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma; au
- Imechapishwa kwa idhini ya ushirika na pale inapohitajika chini ya Mkataba wa Bidhaa/Kazi/Huduma, na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja.

7.6. Kabla ya kukamilika kwa mradi, hakuna Mwanachama atakayepaswa kutumia picha, au taarifa nyingine inayofafanua Mradi, katika kukuza biashara yake mwenyewe, bila idhini ya Mwanachama mwingine;

7.7. Isipokuwa pale imeelezwa vinginevyo katika Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma, hakimiliki ya nyaraka zilizozalishwa na mmoja wa Wanachama kuhusiana na Mradi zitatolewa kwa Wanachama, na kila Mwanachama atapewa kibali cha kutumia na kuzalisha nakala za nyaraka hizo;

7.8. Isipokuwa kama ilivyoainishwa katika Kifungu Kidogo cha 8.6, Kila Mwanachama atafidia madai, wajibu, uharibifu, gharama na hasara zote za wanachama zilizopatikana kutokana kurudia matumizi ya usanifu, michoro, na nyaraka nyingine zilizotolewa kwa ajili ya Mradi katika miradi mingine.

## 8.0. WAFANYAKAZI

8.1. Kila Mwanachama atatenga idadi ya kutosha ya wafanyakazi wake kwenye Mradi ili masharti ya Makubaliano haya yazingatiwe pamoja na Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma zisambazwe/zijengwe/zitolewe kwa mujibu wa Mkataba. Isipokuwa kama imekubaliwa vinginevyo, Ushirika hauna wafanyakazi wake wenyewe;

8.2. Kila Mwanachama atawajibika kwa matendo yote ya wafanyakazi wake na ataendelea kuwajibika kwa namna zote kama mwajiri wa wafanyakazi wake;

8.3. Bila kujali masharti yaliyoainishwa katika Kifungu kidogo kilichopita cha kifungu hiki, Kila Mwanachama anaweza kuruhusu mtu, kampuni au shirika lolote ambalo anaudhibiti nao; kwa kuzingatia idhini ya Wanachama wengine, kutimiza wajibu wowote ambao ni wajibu uliotolewa katika Makubaliano haya, katika mazingira hayo, udhibiti na uwajibikaji kwa wajibu huo wakati wote utabaki chini ya Mwanachama huyo;

8.4. Kila Mwanachama anaweza kuwa na haki ya kualika, kwa kutegemea idhini ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja (ikiwa inahitajika) na kwa makubaliano ya Wanachama, mkandarasi mdogo ili kutekeleza wajibu wowote wa Mwanachama huyo, isipokuwa kwamba katika mazingira hayo udhibiti na wajibu wa kutekeleza majukumu hayo wakati wote utabaki kwa Mwanachama husika;

## 9.0. WAJIBU NA WATU WENGINE

9.1. Hakuna Mwanachama atakayepaswa kuuza, kutoa, kuwekeza kama dhamana, kuweka ahadi, kuhamisha au kwa namna yoyote kuondosha haki au maslahi yoyote chini ya Makubaliano haya, au maslahi yake katika fedha zozote zinazolipika na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja isipokuwa kwa mabadiliko yanayofaa benki

9.2. zake kuhusu fedha yoyote inayodaiwa au itakayodaiwa chini ya makubaliano ya mkataba wa Bidhaa/Kazi ujenzi/Huduma, bila idhini ya maandishi ya awali ya Wanachama

9.3. Makubaliano haya ni kwa faida ya Wajumbe pekee na hayapaswi kutafsiriwa kwamba yanatoa, iwapo ni moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja, haki au sababu za kuchukua hatua kwa watu wengine

## 10.0. UTEKELEZAJI WA VIFUNGU

10.1. Iwapo sehemu yoyote ya kifungu chochote cha Mkataba huu itaonekana na mpatanishi, Mahakama, au mamlaka nyingine yenye uwezo, kuwa batili au haiwezi kutekelezwa, sehemu hiyo ya kifungu itachukuliwa kuondolewa katika Makubaliano haya, na sehemu nyingine za kifungu hicho pamoja na vifungu vilivyo baki vya Makubaliano haya vitaendelea kuwa na nguvu na kutekelezeka kikamilifu.

10.2. Bila kujali kifungu kidogo cha 11.1, Wanachama watajadiliana kwa uaminifu ili kukubaliana kuhusu masharti ya kifungu kilichoridhiwa na pande zote kitakachochukua nafasi ya sehemu ya kifungu kilichobainika kuwa batili au hakiwezi kutekelezwa.

## 11.0. MWANACHAMA ALIYEKIUKA MASHARTI

11.1. Pale inpotokea hali ya kufilisika kwa mwanachama, mwanachama mwingine [au wanachama waliobaki katika Ushirika] atamwakilisha na kuteuliwa rasmi kumwakilisha mwanachama huyo katika masuala yote yanayohusiana na utekelezaji wa Makubaliano haya.

11.2. Mwanachama ambaye atachelewesha au kushindwa kutimiza majukumu yake kwa sehemu au kwa jumla chini ya Makubaliano haya atachukuliwa kuwa amekiuka na atalipa fidia kwa Mwanachama/wanachama wengine kutokana na matokeo ya ukiukwaji huo

11.3. Taarifa kwa maandishi kutoka kwa Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kwamba utekelezaji wa majukumu chini ya Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma haukidhi matarajio au kwamba ushiriki wa Mwanachama hauna umuhimu zaidi kwa sehemu au kwa

jumla, kwa madhumuni ya Kifungu hiki, itamaanisha kwamba Mwanachama husika yuko katika ukiukwaji isipokuwa imekubaliwa vinginevyo na Mwanachama/wanachama wengine.

11.4. Iwapo ukiukwaji wa Mwanachama utakuwa kwamba, mwanachama husika kwa kiasi kikubwa amevunja wajibu wake ulioainishwa katika makubaliano haya, Mwanachama mwingine (au wengine) atakuwa na haki ya kupanga upya kazi husika.

11.5. Hatua zozote zilizochukuliwa na Mwanachama mwingine dhidi ya Mwanachama aliyekiuka makubaliano kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 12.4 hapo juu hazitaathiri haki yoyote ambayo anaweza kuwa nayo kisheria dhidi ya Mwanachama anayekiuka makubaliano

11.6. Iwapo kazi itapangwa upya chini ya Mkataba wa bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma imetekelezwa kwa mujibu wa Kifungu hiki, Mwanachama aliyekiuka haki yake hatamzuia Mwanachama anayefanya kazi iliyopangwa upya na atahakikisha anampatia nyaraka zote na taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi husika.

11.7. Kiasi chochote kilikachopokelewa na Ushirika kama malipo ya wajibu wa Mwanachama aliyeshindwa kutimiza wajibu wake kimeshachukuliwa, kitatumika kulipia hasara yoyote au uharibifu uliosababishwa na kushindwa kutimiza wajibu huo. Mwanachama aliyekiuka atabaki kuwa na wajibu wa kutoa dhamana na bima zinazohusiana na wajibu uliogawanywa kwa mwanachama huyo kabla ya kugawanywa upya, hadi kumalizika kwa Bidhaa/Ujenzi/Huduma

11.8. Iwapo majukumu yote ya Mwanachama aliyekiuka yatapangwa upya kwa mujibu wa kifungu hiki, Mwanachama mwingine/wengine watakuwa na haki na atalazimika:-

11.8.1. Kuendelea na kukamilisha utekelezaji wa Mkataba wa bidhaa/Kazi za ujenzi/ Huduma bila ushiriki wa Mwanachama aliyekiuka makubaliano, warithi wake, wapokeaji au wawakilishi wengine wa kisheria na ataendelea kuchukua hatua kwa mujibu wa masharti ya Makubaliano haya (kama yalivyorekebishwa ili kuzingatia kutoshiriki kwa Mwanachama aliyekiuka makubaliano); na

11.8.2. Kuzihifadhi kwa ajili ya utekelezaji wa Mkataba wa bidhaa/Kazi/Huduma vifaa vyote na malighafi zote zilizonunuliwa kutokana na mkataba huo na mali zote zinazomilikiwa na Ushirika katika kipindi cha ukiukwaji wa wajibu na Mwanachama hadi kukamilika kwa usambazaji wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma

11.8.3. Mwanachama aliyekiuka masharti, warithi, wapokeaji au wawakilishi wake wengine wa kisheria watatekeleza na kufanya masuala yote, kuwasilisha nyaraka na vitu vyote muhimu vitakavyowezesha vifaa na mali zilivyotajwa kuendelea kutumika na kuwezesha Ushirika kuendelea bila ushiriki wa Mwanachama aliyekiuka masharti

11.9. Baada ya kukamilika au kusitishwa mapema kwa Mkataba wa Bidhaa/Kazi za ujenzi/Huduma na kupokelewa kwa kiasi chote kinachotakiwa kulingana na mkataba huo, Mwanachama aliyebaki atalipa hesabu kwa Mwanachama aliyekiuka masharti ambaye atakuwa na haki ya kupokea kiasi sawa na fedha yoyote iliyotolewa na Mwanachama aliyekiuka kuelekea katika fedha za jumla ambazo hazijatumika awali, pamoja na sehemu ya Mwanachama huyo katika fedha zozote za Ushirika zinazomuhusu,zitatolewa pungufu kutokana na hasara au uharibifu uliojitokeza kutokana na ukiukwaji wake

11.10. Iwapo sehemu ya hasara inayolipishwa na Mwanachama anayekiuka itazidi kiasi chochote kilichotolewa na Mwanachama huyo kwa fedha za jumla na sehemu ya fedha yoyote ya Ushirika inayomilikiwa kwake kwa mujibu wa masharti ya Makubaliano haya, Mwanachama aliyekiuka atalipa mara moja kiwango kilichozidi kwa Mwanachama/Wanachama wengine

## 12.0. MUDA WA MAKUBALIANO WA USHIRIKA

12.1. Ikiwa imeamuliwa kwa pamoja na Wanachama kwamba Zabuni haitakubaliwa na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja au ikiwa haitakubaliwa na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja ndani ya kipindi kilichowekwa kwa ajili ya kukubaliwa kwa mujibu wa Zabuni au kuongezeka kokote kwa kipindi hicho kilichokubaliwa baadaye kati ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja na Ushirika, Makubaliano haya yatasitishwa mara moja

12.2. Ikiwa Zabuni itakubaliwa na Mnunuzi/Mwajiri/Mteja, Makubaliano haya yataendelea kuwa na nguvu kamili na kuendelea kutekelezwa vilevile wakati wa Mkataba wa usambazaji wa Bidhaa/ ujenzi/utoaji huduma umeingiwa kati ya Mnunuzi/Mwajiri/Mteja, hadi uthibitisho utakapopokelewa kutoka kwa

Mnunuzi/Mwajiri/Mteja kwamba Usambazaji wa Bidhaa/ujenzi/utoaji Huduma umekamilika, au umefutwa, na akaunti zote zinazohusiana na Huduma kati ya Ushirika, Mteja na wahusika wengine na kati ya Wanachama zinatambuliwa kama zimelipwa

Pale ambapo masharti ya Makubaliano haya yataendelea kuwawajibisha Wanachama kwa kiwango na muda unaohitajika katika utekelezaji wa haki na wajibu ulioainishwa katika Makubaliano.

## 13.0. WAJIBU WA WANACHAMA KWA USHIRIKA

13.1. Wanachama wanaelewa na kukubaliana kwamba kila Mwanachama atawajibika binafsi kwa ukiukwaji wowote unahusiana na utekelezaji wa majukumu yake kulingana na masharti na vigezo vya Makubaliano haya.

13.2. Kila Mwanachama anathibitisha kwamba atalipa fidia na kuendelea kulipa fidia kwa Mwanachama mwingine/wengine dhidi ya wajibu wote wa kisheria unatokana na utekelezaji, au vinginevyo, wajibu wake chini ya Makubaliano haya.

13.3. Iwapo mmoja wa mwanachama atatuhumiwa kwa maandishi kwamba wajibu wowote wa kisheria umechangiwa na Mwanachama au Wanachama wengine waliobaki, Wanachama watatumia jitihada za busara kufikia makubaliano kuhusu wajibu ambao kila Mwanachama atabeba, na iwapo Wanachama watashindwa kufikia makubaliano hayo, mgawanyo sahihi utaamuliwa kwa njia ya upatanisho kwa mujibu wa Kifungu cha 19

## 14.0. BIMA

14.1. Isipokuwa Wanachama wamekubaliana vinginevyo, kila Mwanachama atapaswa kuweka jitihada kuwa na bima kama kinga dhidi ya wajibu wote wa kisheria unaotokana au kuhusiana na utekelezaji, au vinginevyo, wajibu wake chini ya Makubaliano haya.

14.2. Kila Mwanachama atafanya jitihada zote kuwa na bima kwa ajili ya umma/uwajibikaji kwa watu wengine na bima nyingine yoyote inayohitajika ili kukidhi masharti ya Mkataba wa Usambazaji bidhaa/Kazi za ujenzi/utoaji Huduma.

## 15.0. GHARAMA ZA UHAMASISHAJI NA MRADI, FAIDA, HASARA NA STAHIKI

15.1. Kila Mwanachama atarudishiwa gharama na matumizi aliyoyatumia kuhusiana na uhamasishaji, maandalizi, majadiliano na uwasilishaji wa zabuni, kulingana na gharama halisi kama ilivyoainishwa katika jedwali la 3.

